# Nipashe

Jumatatu Februari 1, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580478

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Serikali** yasisitiza hadhari dhidi ya corona

UKURASA 2



**Wanafunzi** 27 wapigwa na radi wakisoma darasani

UKURASA 3



**Wanasoka nyota 10 wenye wafuasi wengi Instagram**

UKURASA 12

# JPM awatangazia utumbuaji ma-DC

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**BABA ADAIWA KUNAJISI MWANAYE WA MIAKA 3**

WATU wawili wakazi wa Jiji la Arusha, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi...

UKURASA WA 5

**EPZ YAPEWA MAAGIZO UJENZI WA VIWANDA**

Waziri aipa EPZ maagizo ikipata mkurugenzi mpya Serikali kupitia...


## Maalim Seif ni mgonjwa, yasema ACT-Wazalendo

UKURASA 3



Rais Dk. John Magufuli, akizungumza jambo na watoto ambao majina yao hayakupatikana mara moja, baada ya kuwahutubia wananchi wa Manyoni mjini, mkoani Singida, jana. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store




RIPOTI MAALUM

## Madhila yanayokumba wagonjwa hospitalini

UKURASA 4

**MICHEZO** **FISTON WA YANGA ATAJWA SIMBA** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

## Serikali yasisitiza hadhari ya corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari zote za kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19) huku ikiahidi kuwa haita wafungia ndani wananchi wake.

Msemaji Mkuu wa serikali Dk, Hassan Abbasi, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mambo mbalimbali katika kipindi cha miaka mitano ya awamu ya pili.

Alisema msimamo wa serikali ni kutowafungia watu ndani katika kipindi hicho ambapo pamekuwa na taarifa za mlipuko wa ugonjwa huo katika mataifa jirani na Tanzania.

"Kama ambavyo Rais Magufuli, alivyosema katika moja ya ziara yake kuwa hakuna mtu atakae fungiwa ndani bali wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhali zote za kujilinda wenyewe," alisema.

Pia, alisema kuwa msimamo wa serikali ni kutowafungia watu ndani lakini kama kuna mtu anafikiri vinginevyo ajifungie ndani mwenyewe.

"Hatuta fungia mtu ndani watu waendele kufanya shughuli zao za kilimo, michezo, musiki na mambo mengine ya uzalishaji mali na kama kuna mtu anataka kujifungia ajifungie mwenyewe ndani lakini sisi kama serikali hatuta fanya hivyo," alisisitiza Dk. Abbasi.

Alisema katika ziara za Rais Magufuli amekuwa akisisitiza masuala muhimu kwa Taifa kama vile kuendelea kuenzi amani, kulipa kodi, usimamizi imara wa miradi na Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari lakini kutotishwa wala kuchomekewa mawazo au mikakati na watu wengine katika kupambana na UVIKO-19 (COVID-19).

Dk. Abbasi alisema nchi ya Tanzania imeendelea kuwa na heshima katika taswira ya kimataifa kutokana na historia lakini zaidi ni misimamo thabiti ya Rais Magufuli, katika masuala mbalimbali ya kimataifa.

Alisema kutoka na hali hiyo Rais Magufuli amechaguliwa na Waafrika kote Duniani kushika nafasi ya pili katika viongozi 54 wa Afrika kuwa kiongozi Bora wa Kisiasa wa Mwaka Barani Afrika (African Political Leader of the Year 2020) kwa mujibu wa Jarida la AFRICA LEADERSHIP MAGAZINE (ALM).

# Magufuli atishia kuwatema ma-DC

**Na Christina Mwakangale**

RAIS John Magufuli, amesema hatasita kuwaondoa mara moja wakuu wa wilaya zote ambao maeneo yao yatakumbwa na njaa mwaka huu.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kwenye maeneo yao kwa kulima mazao ya aina tofauti.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, akirejea kutoka kwenye ziara ya kikazi mikoa ya Geita, Shinyanga na Tabora.

"Hakuna chakula cha bure sitatoa chakula kwenye wilaya yeyote, wilaya itakayopata njaa, mkuu wa wilaya na yeye ataondoka pia na viongozi ambao wanazembea kuwahamasisha wananchi kufanyakazi.

Usiyefanya kazi usile, hakuna cha bure. Asiyefanya kazi na asile. Fedha tunayopata ikaendelee kujenga miradi ya SGR (Reli ya Kisasa)," alisema.

"Kazi ya serikali kujenga hospitali, kununua ndege, dawa, reli na mengine ya maendeleo. Kujilisha ni kazi yako, si kazi ya serikali," alisema Rais Magufuli.

Alisema pamoja na kuona maeneo kadhaa ya wilayani humo, yakiendelea kuwa na mvua, hakuna kilimo kinachoendelea.

"Ukienda Morogoro utakuta kinamama wamepanga viazi. Bahi kuna mvua, lakini sioni mkilima. Nimeshangaa, mama wa miaka 59 anaomba ekari tatu, alime, nilidhani wakuniomba ni kijana wa miaka 18, tena mkampe kesho huyu mama."

Kadhalika, akiwa eneo la Manyoni, mkoani Singida, Rais Magufuli aliwataka wananchi kulima ili kujiongezea kipato.

"Mvua hazina kusubiri, zinaonyesha tulime, barabara hizi zitaleta faida iwapo tutazifanyia kazi, mazao yenu yataliwa maeneo yote sababu barabara ipo," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli alisema wakati mataifa mengine wananchi wao wakijifungia ndani kwa ajili ya corona, ni wakati wa Tanzania kufanya kilimo na kwamba viongozi wa eneo hilo wawahamasishe watu kufanya kazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Dk. Fatuma Mganga, alisema mapato yameongezeka kutoka Sh. milioni 500 hadi Sh. bilioni moja.

Alisema ongezeko hilo limefanya ujenzi wa sekondari kwenye kata mbili ambako hazikuwapo awali, kujengwa.

"Kata ya Nondwa tayari watoto wanasoma na kata ya Mpinga tunamalizia madarasa, tunatarajia hadi Februari yatakuwa yamekamilika," alisema Dk. Mganga.

Aliongeza kuwa mapato ya ndani ya halmashauri hiyo, yamewezesha kutoa mikopo kwa vikundi 33 na kutoa ajira kwa makundi maalum.

"Madarasa 12 yanajengwa kwa wanafunzi waliokosa ambao wamechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza hadi mwezi ujao wataingia darasani."




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akifunga mafunzo kwa waongoza watalii yaliyoendeshwa na mtaalam kutoka Afrika Kusini na jijini Arusha mwishoni mwa wiki, na kudhaminiwa na kampuni ya Superdoll, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono serikali kuongeza idadi ya watalii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

# Baba adaiwa kumnajisi mwanaye wa miaka mitatu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATU wawili wakazi wa Jiji la Arusha wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za unyanyasaji wa kijinsia katika matukio mawili tofauti, likiwamo la baba mzazi kumuingilia kimwili mtoto wake wa miaka (3).

Inadaiwa tukio hilo limemuathiri kwa kumsababishia kutokwa na haja ndogo bila kukoma.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Arusha, Salum Hamduni, alisema tukio la kwanza lilitokea Januari 25, mwaka huu,majira ya saa 4:30 asubuhi Kijiji cha Olosiva Kata ya Olorieni jijini humo na wanamshikilia baba mzazi Olaisi Wavii (46) wa mtoto wa miaka 3 (jina limehifadhiwa),anayetokwa haja ndogo mfululizo.

Alisema siku ya tukio Ofisa Ustawi wa Jamii akiwa katika shughuli zake za kawaida katika kijiji hicho, alibaini mtoto huyo anayesoma shule ya awali katika Shule ya New Life iliyopo Sakina kutokwa na mkojo mfululizo na kutilia shaka.

"Alipogundua hilo na kutilia shaka alitupa taarifa sisi na tukaanza upelelezi mara moja na tulimuhoji mtoto mwenyewe na majirani mbalimbali ndipo tukabaini baba mzazi amehusika katika tukio hilo na tukamkamata," alisema.

Ailisema wanaendelea kumshikilia na uchunguzi wao ukikamilika watapeleka jalada lake Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP) ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Aidha alitoa wito kwa wazazi na walezi mkoani humo, kuwa makini na uangalizi wa karibu kwa watoto wao.

Aliomba pia viongozi wa dini kutoa elimu kwenye nyumba zao za ibada kwa waumini wao kuwakumbusha kuwatendea haki watoto ambao ni viongozi na taifa la kesho.

Kamamda Hamduni alitaja tukio la pili kuwa wanamshikilia Badro Abdallah (38), mkazi wa Sakina jijini humo kwa tuhuma za kumchoma pasi ya umeme mgongoni mtoto wake wa miaka (12) na kumsababishia maumivu makali mwilini mwake.

Alisema mtuhumiwa amekamatwa na anashikiliwa na jeshi hilo, na uchunguzi ukikamilika jalada lake litafikishwa kwa DPP.

## HABARI KITAIFA

# SGR kuwapa ajira vijana 15,000

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

VIJANA 15,000 kutoka mikoa mbalimbali wanatarajia kunufaika na ajira katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR ), kutoka mkoani Mwanza hadi Isaka, mkoani Shinyanga.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, wakati wa kongamano la mpango kazi na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika mradi wa SGR kutoka Mwanza hadi Isaka.

Kadogosa alisema mradi huo utakagharimu Sh. trilioni tatu, utatoa fursa mbalimbali ikiwamo ajira rasmi kwa watu 15,000, huku wengine 75,000 wakipewa ajira za muda mfupi.

Kadogosa alisema faida nyingine ya ujenzi wa mradi huo ni kuzalisha zabuni mbalimbali za usafirishaji, usambazaji wa vifaa vya ujenzi pamoja na kutoa fursa kwa makandarasi wa kampuni ya ukandarasi ili kuwajengea uwezo wa kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa.

"Ili Tanzania iwe ya viwanda, lazima iwe na reli imara, hivyo agizo la utekelezaji wa mradi huo una sababu za msingi za kukidhi matakwa ya makubaliano ya kimkakati, uhusishwaji wa kiteknolojia, kujiandaa na kujenga uwezo wa sisi kujenga," alieleza Kadogosa.

Akizungumzia suala la vishoka wanaoibuka wakati wa utekelezaji wa miradi, alisema watawaondoa kwa ushirikiano na sekta binafsi kwa sababu wanahitaji watu wanaofanya kazi kwa umakini.

Akifungua kongamano hilo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwahakikishia usalama wa kutosha wakati wa ujenzi huo na kusaidia upatikanaji na utatuzi wa changamoto kwa wale watakaokuwa na tatizo.

Alisema wanatekeleza miradi mbalimbali ukiwamo ujenzi wa meli, daraja la Magufuli na ukarabati wa uwanja wa ndege, hivyo kwa mradi wa reli kila mtu aingie kwenye mfumo wa kufuata utaratibu na weledi katika utendaji kazi.

Alisema katika miezi 36 ya utekelezaji mradi huo, wadau mbalimbali na wananchi waione ni fursa ya kuwekeza mkoani humo.

Mkandarasi Mkuu wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction inayojenga mradi huo, Junle Zhang, alisema watatekeleza mradi huo kwa weledi na watahakikisha kuwa wanaukamilisha ndani ya muda uliopangwa.



Mbunge wa Kiteto mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita, akivishwa vazi la asili la wafugaji kwenye harambee ya ujenzi wa Shule ya Aawali Orpirkata Kijiji cha Namelock, ambapo zaidi ya Sh. milioni 8 zilipatikana jana. **PICHA: GIFT THADEY.**

# Maalim Seif mgonjwa, yasema ACT Wazalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAARIFA za kuugua kwa Makamu wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maalim Sef Sharif Hamad, jana ziliibua mshtuko miongoni mwa wananchi.

Hali hiyo ilitokana na kusambaa kwa taarifa za Maalim Seif, ambaye chama chake cha ACT-Wazalendo kilijumuishwa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka jana, kwamba amelazwa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Chama chake kilitoa taarifa kikisema kiongozi huyo alifanyiwa vipimo na kugunduliwa kuwa ana ugonjwa..

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na chama hicho, Maalim Seif amepumzishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, huku akiendelea kupatiwa matibabu.

"Tunapenda kuchukua nafasi hii kuujulisha umma kuwa hali ya Maalim Seif pamoja na mkewe zinaendelea vyema kabisa, "alisema Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, katika taarifa hiyo.

Kwa upande wake Kaimu Waziri wa Afya, Simai Muhamed Said, kuwa hana taarifa kuhusiana na ugonjwa inaomsumbua Maalim Seif kama taarifa za mitandao zilivyokuwa zinadai.

"Mimi sina taarifa hizo kabisa, muulizeni huyo aliyetoa taarifa,"alisema Simai.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambae ndie msemaji wa serikali, Dk. Khalid Salum, alisema hana taarifa hizo na kuwataka wananchi watulie.

# Wanafunzi 27 wajeruhiwa na radi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WANAFUNZI 27 wamejeruhiwa na radi na kupelekwa Hospitali ya Rufani ya mkoa Kagera. Radi hiyo ilisababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Museleta Nyakiloto, alithibitisha kupokea majeruhi hao juzi kutoka Shule ya Sekondari Kalema, Tarafa ya Bugabo, wilaya ya Bukoba majira ya sita mchana.

Nyakiloto alisema katika majeruhi hao wavulana ni wanane na wasichana 19, na kwamba hali zao zinaendelea vizuri.

Akizungumzia tukio hilo, mwanafunzi wa kidato cha nne aliyekuwa katika darasa ambalo majeruhi wamepigiwa na radi, Darius Medard, alisema, juzi majira ya saa tatu asubuhi wakiwa darasani wakisoma somo la Historia, radi ilipiga hivyo kuanza kikimbia kutoka nje. "Radi ilivyopiga tu tulianza kukimbia nje kutoka darasani tulipokuwa tumeungana mikondo mitatu A,B na C, ndipo wanafunzi wanane walianguka chini tukawabeba kuwaweka nje mkuu wa shule akasema tuwamwagie maji," Alisa Medard.

"Wengine walidai wanasikia moto kwenye miili yao, baadae gari la wagonjwa likaja kuwabeba na kuwapeleka hospitali. Hadi saa saba mchana walikuwa wamefikia wanafunzi 25 wa kupelekwa hospitali," alisema.

halotel

TAARIFA KWA UMMA

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano, ili kuendelea kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

GHARAMA ZA KUPIGA NCHINI

| Piga kwenda mitandao | Gharama (Tsh/dk) |
|---|---|
| Halotel - Halotel | 60 |
| Halotel - Mitandao yote | 60 |

GHARAMA ZA KUPIGA NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/dk) |
|---|---|
| Ukanda 1: USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| Ukanda 2: Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| Ukanda 3: Rwanda, South Africa, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| Ukanda 4: Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| Ukanda 5: Burundi | 1,350 |
| Ukanda 6: Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| Ukanda 7: Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA SMS

| SMS kwenda | Gharama (Tsh/SMS) |
|---|---|
| SMS ndani ya nchi | 30 |
| SMS kimataifa | 95 |

GHARAMA ZA INTANETI

| Data (MBs) | Gharama |
|---|---|
| MB | 25.6 Tsh/MB |

Halotel Tanzania

Hotline 100

RIPOTI MAALUM

# Madhila yanayokumba wagonjwa hospitalini

■Wazazi waondoka na nguo kwenda kufua nyumbani
■Kila mgonjwa atozwa 10,000 ya kitanda na usajili

Na Dinna Maningo, TARIME

TANZANIA ina Mpango wa Maendeleo ya Afya Msingi (MMAM) ambao pamoja na mambo mengine, unaielekeza serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati na kila kaa iwe na kituo cha afya.

Vivyo hivyo, mpango huo inaitaka serikali kuhakikisha kunakuwa na hospitali ya wilaya katika kila wilaya, hospitali ya rufani kila mkoa na kwenye ngazi ya juu zaidi kitaifa ndiko kuna Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kimsingi, chimbuko la mpango huo ni Sera ya Afya ya Mwaka 1990 iliyorejewa mwaka 2007 ikiitaka serikali kuongeza kasi ya kusogeza huduma bora za afya ya msingi kwa kila mwananchi, ili kuboresha hali ya ustawi wa maisha na kukuza uchumi wa kipato.

Katika kufuatilia utekelezaji wa mpango huo muhimu, Nipashe inafunga safari hadi kwenye Kituo cha Afya Nyangoto kilichoko Nyamongo wilayani Tarime mkoani Mara ambacho wananchi wamekuwa wakilalama kutopata huduma stahiki kutokana na ukosefu wa dawa, gari la wagonjwa, gharama kubwa za matibabu na upungufu wa watumishi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), pia alizuru kituoni huko wiki iliyopita kujionea kinachojiri akifuatana na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi CCM, akiwamo Katibu wa chama hicho wilayani Tarime, Hamis Mkaruka.

Viongozi wengine waliokuwapo kwenye ziara hiyo ni Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya, Marema Sollo, Katibu wa Vijana, Newton Mwongi, Katibu wa Uhamasishaji, Remmy Mkapa, Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Apoo Tindwa, na wataalamu wa masuala mbalimbali kutoka Ofisi ya Halmashauri hiyo.

Akiwa kituoni huko na timu yake hiyo, Waitara ambaye pia ni Mbunge wa Tarime Vijijini, alizungumza na viongozi wa vijiji na kata na kutembelea wodi za wagonjwa.



Veronica Tontora, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Lamboni, akionyesha eneo ambalo limetelekezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, ambalo lilikuwa linatumiwa na wagonjwa na wanaojifungua kufulia nguo zao, lakini kwa sasa halitumiki kwa madai kuwa limeziba. **PICHA: DINNA MANINGO**

### KILICHOBAINIKA

Viongozi hao walibaini kinamama wanaojifungua kituoni huko, wanaondoka na nguo zao kwenda kufua nyumbani.

Pendo Mnata, mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Mjini Kati na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake CCM (UWT) Kata ya Matongo, alisema kinamama wanaojifungua katika kituo hicho, hulazimika kuondoka na nguo zao chafu kwenda kufua nyumbani kwa kuwa kituo hicho hakina chumba na eneo kwa ajili ya kazi hiyo.

"Kuna kipindi kinamama waliojifungua walikuwa wanafua nguo kwenye majani baada ya sinki lililokuwa likitumika kufua nguo kuziba.

"Mwezi wa sita (Juni) mwaka jana, uongozi wa kituo ulizuia watu kufulia kwenye majani. Ikabidi sasa ukijifungua, unaambiwa uende ukafulie kwako.

"Mimi mwenyewe nilimpeleka mkamwana wangu kujifungua, alijifungua kisha akaenda kuoga na tukaambiwa kabisa kuwa 'bafu lililopo ni kwa ajili ya kuoga tu, nguo nendeni mkafue nyumbani'.

"Sasa jamani nguo chafu, tena zenye damu, na (wazazi) wengine unakuta wana matatizo ya uzazi, hawaondoki siku hiyo hiyo, wanalala na hizo nguo zenye damu mpaka atakaporuhusiwa kuondoka au ndugu zake wakimtembelea wanaondoka nazo," Mnata alibainisha.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Lamboni, Veronica Tontora, hakuwa nyuma katika kuwasilisha kilio chao, akisema:

"Kinamama wanaojifungua, wanapata tabu na wagonjwa wengine pia. Kuna mama alijifungua, akaambiwa beba nguo na kondo lako ukafulie nyumbani, tunaomba kituo kiboreshwe."

### SHIDA WANAOPEWA RUFANI

Ziara ya viongozi hao ikabaini kuwapo kwa shida nyingine inayowakabili wagonjwa wanaopewa rufani kutoka kituoni hapo.

Wenyeji walisema licha ya kuwapo kwa gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo hicho, limekuwa halipatikani kituoni muda mwingi, hivyo mgonjwa akipewa rufani, ndugu hulazimika kuchukua magari ya kukodi na wasio.

Wambura Machugu, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kebamonche na mjumbe wa Kamati ya Afya na Mazingira kijijini Mjini Kati, alisema kutokana na kukosekana kwa gari la wagonjwa, baadhi ya wagonjwa wanaopata rufani kwenda Hospitali ya Wilaya, Hospitali ya Rufani ya Mkoa na Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, hufariki dunia kwa kushindwa kumudu gharama za usafiri binafsi.

"Juzi, kuna mgonjwa alilazwa hapa kituoni, alikaa siku mbili na hali yake ilikuwa mbaya, ikatakiwa asafirishwe kwenda mkoani, lakini hapakuwa na gari, hali ikawa mbaya, akafia kituoni hapa.

"Inaumiza kituo kikubwa kama hiki, kina gari lakini gari linakwenda kufanya kazi kwingine ilhali liliietwa kwa matumizi ya kituo hiki," alilalamika.

### DENI LA DAWA

Diwani wa Viti Maalum, Felister Range, alisema: "Hiki kituo kimegeuka kuwa kero kwa wagonjwa. Niliwahi kuleta mgonjwa, hata karatasi ya kuandikia hakuna, nikaambiwa nikanunue daftari nikaleta.

"Haikutosha dawa hazipo, kila kitu unaambiwa kanunue, nilifuatilia hadi ofisi ya DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya), akasema wana upungufu wa dawa kwa kuwa wanadaiwa na MSD (Bohari Kuu ya Dawa) japo sikujua ni la kiasi gani."

Diwani wa Viti Maalum, Elizabeth Marembera, alisema ukosefu wa dawa umesababisha wananchi kugoma kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa kuwa hata walio na bima, hawapati huduma inayostahili na wanalazimika kununua dawa kwa gharama zao licha ya kuwa na bima.

"Wananchi wanashindwa kukata bima kwa sababu hakuna huduma, kila kitu unaandikiwa ukanunue, unanunua dawa, vipimo vingine unaambiwa ukapime huko, ununue bomba la sindano, mgonjwa unakuja usiku saa nane, unaambiwa ukanunue dawa, unaitoa wapi maduka yanakuwa yamefungwa?

"Mtu atashawishikaje kujiunga na bima? Sasa hivi watu wamechukia, wenye fedha wanatibiwa hospitali binafi, watu maskini ndiyo wanateseka kwa kukosa huduma." alionya.

Diwani wa Kata ya Matongo, Godfrey Kegoye, alisema kuna upungufu wa wodi ya wanawake katika kituo hicho, hali inayosababisha wagonjwa wawili kulala kwenye kitanda kimoja na baadhi kulala sakafuni.

Alisema kutokana na tatizo hilo, baadhi ya wagonjwa wenye uwezo kifedha, wamekuwa wakilazimika kukikimbia kituo hicho cha serikali na kwenda kumalizia matibabu yao kwenye vituo vya taasisi binafsi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kituo cha Afya Nyangoto, Isaack Zabroni, alisema ni mwaka mmoja sasa eneo lililotengwa kwa ajili ya kufua nguo za wanaojifungua na wagonjwa halitumiki.

Tofauti na ilivyodaiwa na wazungumzaji wa awali, kiongozi huyo alisema nguo za wagonjwa zimekuwa zikifuliwa kwenye bafu la kituo hicho na kwamba hakuna kinamama wanaokwenda kufua nguo nyumbani.

"Ni mwaka mmoja sinki halitumiki, lilitengenezwa chini ya kiwango na kampuni iliyopewa zabuni ya kufanya usafi kwenye kituo hiki cha afya, waliweka tundu dogo likaziba.

"Ili lizibuliwe, kunahitajika lichimbwe shimo ambao watu wakifua maji yatatiririka kwenda ndani ya shimo tofauti na hapo hata likizibuliwa litachukua muda mfupi litaziba tena," alifafanua.

Akizungumzia ukosefu wa dawa, mwenyekiti huyo alikiri MSD iliingia mkataba na serikali na sasa kuna fedha za dawa hawajazilipia kwa muda mrefu.

"Kuna baadhi ya wauguzi walikuwa wanakuja kazini wakiwa na mabegi yenye dawa, hii ilitupa wasiwasi je, kweli ni dawa zao binafsi au wanachukua kituoni?

"Ilitubidi tuzuie huo utaratibu, tukakataa 'hakuna nesi kumwelekeza mgonjwa duka la kununua dawa au muuguzi yeyote kuuza dawa na wengine walihamishwa," alisema.

ITAENDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

# Mfumo waja kudhibiti migogoro sehemu za kazi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI imezindua rasmi mpango wa kusikiliza na kushughulikia taarifa za malalamiko ya sekta ya kazi na ajira ili kuwadhibiti baadhi ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi wasio waaminifu wanaotumia madaraka yao vibaya ili kujipatia rushwa pale inapotokea migogoro kati ya wafanyakazi na waajiri.

Kupitia mpango huo, Serikali Imeunda kikosi kazi cha kufanya ukaguzi maalumu katika sekta ya kazi na ajira chenye lengo la kutatua changamoto wanazokabiliana nazo na kuhakikisha kunakuwa na mazingira rafiki kwa wafanyakazi, waajiri na wadau wengine.

Uzinduzi huo ulifanyika Manispaa ya Morogoro kuhudhuriwa na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, viongozi wa vyama vya waajiri, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), watendaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo za WCF,NSSF,PSSSF,OSHA na CMA na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Sanare.

Akizindua mpango huo,Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge,Kazi,Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema ni sawa na kliniki ya awali ya kusaidia wafanyakazi, waajiri na wananchi kuzungumza matatizo yao kabla ya kufikishwa kwenye vyombo vya juu vya uamuzi.

Alisema lengo lingine la kliniki hiyo ni kuwasaidia wadau hao kwa pamoja kufahamu mamlaka sahihi ya kuwasilisha malalamiko yanayohusu sekta hizo ili ziweze kupatiwa ufumbuzi wa kina baada ya kushindwa kuafikiana katika kliniki hiyo.

# Waziri aipa EPZ maagizo ikipata mkurugenzi mpya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imemteua John Mnali kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), akichukua nafasi ya Kanali Mstaafu Joseph Simbakalia.

Mnali ambaye atakaimu nafasi ya Mkurugenzi Mkuu anakabiliwa na jukumu zito la kuijenga taasisi kuwa imara zaidi na kuongoza katika juhudi za kujenga uchumi wa viwanda nchini.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati wa makabidhiano ya ofisi na kusisitiza kuelewa matazamio ya serikali na nafasi ya pekee ya taasisi ya EPZA katika ujenzi wa viwanda.

"Mkurugenzi mpya anatakiwa kutengeneza mpango mkakati ili kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo yapo chini ya EPZA na hayajaendelezwa yaweze kujengwa miundombinu itakayoweza kuwavutia wawekezaji katika viwanda," alisema.

Alisema ili kufikia maendeleoa endelevu, ni jukumu la EPZA chini ya mkurugenzi mpya kutenga maeneo maalum ya ukanda wa kiuchumi yakiwa yametengenezewa miundombinu rafiki kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji katika viwanda.

Aliitaka EPZA kushirikiana na halmashauri za wilaya kutenga maeneo ya ukanda maalum ya uwekezaji na kuweza kuyaendeleza kwa pamoja ili kugawana mapato yatakayopatikana kutokana uwekezaji.

Naibu Waziri Kagahe alimpongeza Mkurugenzi aliyemaliza muda wake, Simbakalia kwa kazi Kubwa aliyofanya ya kuibadilisha taasisi iweze kuchangia zaidi katika ujenzi wa viwanda nchini.

Alisema Simbakalia amefanya kazi kama Mkurugenzi Mkuu kwa zaidi ya miaka sita, japo alipewa mkataba wa miaka mitano iliyotamatika mwaka 2019.

"Alisema kuwa serikali ilimuongezea muda mara baada ya mkataba wake kufikia kikomo wakati ikiwa inatafuta atakayechukua nafasi yake. Pamoja na hiyo, Simbakalia amefanya kazi iliyotukuka katika kipindi chake," alieleza.

Aliwataka wafanyakazi wa EPZA kufanya kazi kwa bidii na uaminifu na wale watakaokiuka maadili wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Kwa upande wake, Mnali aliwataka wafanyakazi wa EPZA kumpa ushirikiano katika utendaji wa kazi katika taasisi ili malengo na matazamio ya serikali ya kujenga Uchumi Mkubwa wa viwanda yaweze kutimia.

"Matarajio ya serikali katika taasisi ya EPZA kwenye ujenzi wa viwanda ni makubwa sana hivyo kila mmoja wetu anajukumu la kutoa mchango wake ili kufikia azma hii," alisema.

Pia Mnali amemuahidi Naibu Waziri Kagahe kuwa atatekeleza maagizo yote ambayo amempa katika kuhakikisha EPZA inakuwa kinara katika kutimiza lengo la serikali la ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Naye Simbakalia alimtaka Mkurugenzi mpya wa EPZA kuhakikisha kuwa anatekeleza majukumu yake kwa kufuata sharia zinazoingoza taasisi ili kuweza kuwavutia wawekezaji zaidi.


## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

1st Housing

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12. 2020

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Dec. 2020 | Robo Mwaka iliyopita 30th Sep. 2020 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2 | 2,347 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 2,542,147 | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 8,903,725 | 11,679,329 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 6,301,150 | 4,977,466 |
| 12 | Mali Nyingine | 593,994 | 610,370 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 247,026 | 375,962 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **20,210,045** | **19,267,475** |
| | | | |
| B. | B. **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 404,366 | 404,366 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 753,177 | 716,183 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 87,558 | 76,510 |
| 27 | Dhima Nyingine | 11,712 | 1,459 |
| 28 | Madeni | 1,010,479 | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **2,267,293** | **1,198,519** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **17,942,752** | **18,068,956** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,424,068) | (3,424,068) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (529,011) | (402,808) |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **17,942,752** | **18,068,956** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | - | - |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 55,828 | 55,828 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 88.78% | 93.78% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.00% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1550.44% | 1225.27% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 31.18% | 25.83% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.99% | 88.85% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.00% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4.89% | -0.91% |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2020 | 31st Dec. 2019 | 31st Dec. 2020 | 31st Dec. 2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 418,484 | 355,105 | 1,566,825 | 908,437 |
| 2 | Gharama za Riba | (15,576) | (46,581) | (35,911) | (60,415) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **402,909** | **308,524** | **1,530,914** | **848,022** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 0 | (70,475) | 30,303 | 18,539 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **49,804** | **41,691** | **68,283** | **63,497** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1 | (4,156) | (2,622) | (3,719) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 46,233 | (1,711) | 51,933 | 7,850 |
| | 6.3 Gawio | - | (1) | 10,333 | 11,807 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 3,571 | 47,559 | 8,640 | 47,559 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(578,916)** | **(511,896)** | **(2,157,478)** | **(2,036,474)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (176,160) | (222,419) | (873,061) | (861,881) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (402,757) | (289,478) | (1,284,417) | (1,174,593) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(126,204)** | **(232,157)** | **(527,978)** | **(1,106,416)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | (4,606) | (1,033) | (5,787) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(126,204)** | **(236,763)** | **(529,011)** | **(1,112,203)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | 95,831 | - | 95,831 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **(126,204)** | **(140,932)** | **(529,011)** | **(1,016,372)** |
| | | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 12 | 11 | 12 | 11 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.58) | (0.39) | (2.43) | (5.10) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.64% | -0.77% | -2.65% | -4.97% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -0.70% | -0.82% | -2.91% | -5.35% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 127.88% | 146.17% | 134.91% | 209.53% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.39% | 2.01% | 9.21% | 8.86% |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.12.2020)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.10.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,826,875)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,068,956** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (126,204) | - | - | - | (126,204) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,953,079)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,942,752** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (30.09.2020)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.07.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,736,472)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,159,359** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (90,403) | - | - | - | **(90,403)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.09.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,826,875)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,068,956** |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Jina na Cheo :** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | 25.01.2021 |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | 25.01.2021 |
| Derrick Rushekya **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | 25.01.2021 |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2020 | 30th Sept. 2020 | 31st Dec. 2020 | 31st Dec. 2019 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(126,204)** | **(90,403)** | **(529,011)** | **(1,106,416)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 128,936 | 112,954 | 682,758 | 549,039 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,323,684) | (1,755,103) | (4,433,184) | (1,105,208) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | - | - | 54,203 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (2,542,147) | - | (2,542,147) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,544) | (6,250) | 1,239 | (100,774) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 52,084 | 9,995 | (5,277) | (60,771) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | (4,646) |
| | - Mengineyo | 97,541 | (9,745) | 96,882 | (333,887) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(3,715,019)*** | ***(1,738,552)*** | ***(6,728,741)*** | ***(2,108,460)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | 10,627 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (7,263) | (7,263) | (68,140) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | (485,098) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | (2,028) | (2,028) | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | - | ***(9,291)*** | ***(9,291)*** | ***(542,611)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,010,479 | - | 1,010,479 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (73,409) | (73,409) | (293,638) | (142,239) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***937,070*** | ***(73,409)*** | ***716,842*** | ***(142,239)*** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **(2,777,949)** | **(1,821,253)** | **(6,021,191)** | **(2,793,310)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | 11,681,676 | 13,472,059 | 14,894,048 | 17,668,720 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | - | 30,870 | 30,870 | 18,638 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **8,903,728** | **11,681,676** | **8,903,728** | **14,894,048** |

#### MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| **Jina:** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Sanjay Suchak **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | 25.01.2021 |
| Charles Itembe **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | 25.01.2021 |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Viporo Simba, Namungo vitumike kujimulika CAF*

BAADA ya Ligi Kuu Bara kusimama kwa muda kupisha Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazoendelea nchini Cameroon, hatimaye sasa itaanza kutimua vumbi Alhamisi Februari 4, wiki hii.

Ligi hiyo inarejea baada ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kushindwa kusonga mbele hatua ya robo fainali ya michuano ya CHAN, hivyo kurejea nyumbani na wachezaji wa kikosi hicho kila mmoja kujiunga na klabu yake.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Almas Kasongo, ratiba ya kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, itaanza kwa kuchezwa viporo vinne vya mzunguko wa kwanza vitakavyozihusisha Simba, Namungo, Azam FC, KMC FC na Ruvu Shooting.

Kuwapo kwa viporo hivyo, kulisababishwa na Simba na Namungo ambazo zinaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, kukabiliwa na ratiba ngumu.

Hata hivyo, ligi hiyo inarejea zikiwa zimebaki takribani wiki moja kabla ya Simba na Namungo kurejea tena kwenye michuano ya kimataifa baada ya kufanikiwa kusonga mbele.

Ratiba hiyo ya viporo vya Ligi Kuu inaonyesha Simba ambayo inaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, itashuka katika Uwanja wa Jamhuri Alhamisi wiki hii kuvaana na wenyeji, Dodoma Jiji wakati siku hiyo hiyo KMC FC ikiikaribisha Namungo FC kwenye Dimba la Uhuru jijini Dar es Salaam.

Siku tatu baadaye, Februari 7, Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuikaribisha Azam FC huku Namungo ambayo inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, siku hiyo ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Dimba la Majaliwa mkoani Lindi.

Simba itacheza mechi hiyo dhidi ya Azam ikiwa ni siku tano kabla ya kushuka dimbani nchini DR Congo kuvaana na AS Vita katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Namungo yenyewe ikiwa ni wiki moja kabla ya kuifuata Clube Desportivo de Agosto ya Angola kwenye mechi yao ya awali ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hivyo, pamoja na maandalizi ambayo timu hizo zimeyafanya kwa kucheza mechi kadhaa za kirafiki hususan Simba ambayo ilianzisha michuano ya Simba Super Cup iliyoshirikisha timu tatu; TP Mazembe ya DR Congo na Al Hilal ya Sudan, ikiwa ni maalum kwa ajili ya kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika, bado tunaamini kuna marekebisho ambayo Kocha Mkuu, Didier Gomes, ameyaona na anahitaji mechi zaidi ili kuyafanyia kazi.


Kwa mantiki hiyo, kurejea kwa Ligi Kuu, na wawakilishi hao wa nchi kuanza kwa kucheza viporo vyao, ni wazi kabisa kutatoa nafasi kubwa kwa Gomes wa Simba na Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco, kufanyia kazi makosa ama udhaifu walioubaini katika mechi zao za kirafiki walizocheza kabla ya kuanza mbio hizo za michuano ya CAF.

Gomes ambaye hiyo ndio itakuwa mechi yake ya kwanza Ligi Kuu kuiongoza Simba, tunaamini michezo hiyo miwili ya viporo, itakuwa sahihi kwake kubaini ni eneo gani anapaswa kulifanyia kazi kabla ya kwenda kuivaa AS Vita, na kama timu hizo zitatumia vema michezo hiyo ni wazi kabisa inaweza kuwa chanzo cha kupata matokeo mazuri zitakapokwenda katika majukumu hayo mazito ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# *Ligi inarejea, binafsi sitarajii kusikia visingizio hivi tena*

**WIKI** nzima sasa nimeona kuna baadhi ya timu za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza zikicheza mechi za kujipima nguvu kujiandaa na mechi zinazokuja, hii ina maana timu zimeshajiandaa kisawasawa na mechi zilizobaki.

Baada ya ligi kusimama tangu Januari 3, Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea Fabruari 4, mwaka huu kwa ajili ya kusaka bingwa wa msimu wa 2020/21, huku nne zikishuka daraja moja kwa moja.

Wakati Ligi Kuu ikiwa imesimama, timu za Simba, Yanga, Namungo, Mtibwa Sugar zilikwenda kucheza Kombe la Mapimduzi. Baadhi ya timu zikiwa zinajaribu wachezaji wake wapya ili kuona kama wana viwango vya kuridhisha vya kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza au la.

Timu ya Simba yenyewe ilimpokea Kocha Mpya, Didier Gomes Da Rosa, Mfaransa ambaye amekuja kwenye wakati mzuri ambapo yameandaliwa mashindano mafupi ambayo yamemfanya kuanza kuwajua wachezaji wake kabla hata ligi haijaanza.

Vinginevyo kocha huyo angeanza moja kwa moja na ligi, huku akiwa bado hajawalewa vema wachezaji wake. Kocha huyo pia angekuwa kwenye changamoto kubwa kwani amewakuta wachezaji wa zamani wa timu hiyo, wengine ndiyo kwanza wamesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, huku wengine wakisajiliwa yeye akiwapo.

Michuano ya Simba Super Cup kwa mujibu wake, yamemrahisishia kazi ya kuwatambua wachezaji, hivyo ligi inaanza akiwa hana wasiwasi wa nani anaanze nani asubiri. Kuna timu ambazo muda wote huu hazikuwa na mashindano yoyote yale. Na baadhi zilikuwa zimeshasajili wachezaji kwenye kipindi cha dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu.

Mapumziko yaliyopatikana kwa kiasi kikubwa, yametoa fursa kwa wachezaji wapya kupata muunganiko wa wenzao kwa makocha ambao wako makini na wameanza maandalizi mapema.

Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila yeye amesema kuwa kipindi hiki cha mapumziko ya ligi, amepata muda mzuri wa kuwatengeneza wachezaji wake kwenye utimamu wa mwili, lakini pia kuwafanya wale waliosajiliwa dirisha dogo wazoeane na wenzao.

"Unajua tulisajili wachezaji dirisha dogo, sasa kipindi hiki cha mapumziko kazi yangu ilikuwa kuwaweka sawa kwenye fiziki ili wawe sawa na wenzao waweze kwenda pamoja," anasema kocha huyo.

Hiki kilikuwa kipindi kigumu sana, kwani hakukuwa na maandalizi makubwa sana kwa ajili ya msimu huu wa ligi kutokana na kuibuka ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Nafikiri kila kocha alikuwa kwenye jukumu la kuinoa timu yake ili ifanye vema kwenye mechi zilizobaki za Ligi Kuu na si vinginevyo. Nitashangaa sana nikisikia kocha yeyote akilia na maandalizi, wakati kulikuwa na mwezi mzima wa mapumziko.

Kwa sasa nadhani makocha kama wakipoteza mechi au kufanya vibaya, labda tatizo liwe kwa waamuzi, uwezo mdogo na uzembe wa wachezaji wao, makosa ya kiufundi au matatizo ya uongozi kama vile wachezaji kukosa ari kutokana na kukosa posho au mishahara na si maandalizi.

Kocha yeyote ambaye atakuja mbele ya kamera ya wanahabari na kudai hakuwa na muda wa maandalizi kwenye mechi zilizobaki za Ligi Kuu, sidhani kama ataeleweka si kwa mashabiki wa soka tu nchini, bali hata kwa waajiri wake.

HABARI KITAIFA

# Askari waopoa mwili wa mvuvi Ziwa Victoria

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ASKARI wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Kagera, wameopoa mwili wa Enock Kaiza (27), mzaliwa wa kijiji Mushabagu wilayani Muleba, aliyekuwa akifanya shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Kamanda wa jeshi hilo mkoani Kagera, Thomas Majuto, alisema Januari 30, mwaka huu saa 5:55 asubuhi walipata taarifa kutoka kwa askari polisi kuwa umeonekana mwili wa mtu ukielea juu ya maji katika mwalo wa Nyamkazi Kata Miembeni katika Manispaa ya Bukoba na kwenda kuuopoa.

Majuto alisema taarifa kutoka eneo la tukio zilidai kwamba mvuvi huyo akiwa na mwenzake ambaye hakufahamika jina lake haraka, waliingia ziwani kwa lengo la kuvua samaki Januari 29, mwaka huu, lakini hawakuonekana tena hadi maiti ya mmojawapo ilipoonekana ikielea.

"Inadaiwa waliondoka na mtumbwi wakiwa wawili kwenda kuvua samaki, mvuvi wa pili hajaonekana wala mtumbwi walioondoka nao haujapatikana," alisema Majuto.

Alisema baada ya mwili huo kuopolewa ulipelekwa na kukabidhiwa polisi, kwa ajili ya taratibu nyingine za kiuchunguzi.

Alisema hilo ni tukio la pili la watu kufa maji katika kipindi kisichozidi wiki moja, ambapo Januari 24, mwaka huu mtoto Suleiman Hamidu (10) alikufa baada ya kutumbukia katika dimbwi la maji ya mvua katika eneo la Nshambya katika Manispaa hiyo.

"Tangu mwaka huu uanze matukio ya watu kufa maji hasa katika Ziwa Victoria yalikuwa yamepungua kutokana na elimu ambayo tumepita tukitoa, juu ya umuhimu wa wavuvi na wanaosafiri kupita majini kuwa na vifaa vya kujiokolea inapotokea ajali (maboya), lakini pia tumekuwa tukiwasisitiza kufuatilia taarifa za hali ya hewa kila siku na kuwa na vyombo imara vya majini," alisema.

# Watendaji wabanwa kasi hati za ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri kushiriki zoezi la kuandaa hati za ardhi ili kuongeza kasi ya utoaji hati katika maeneo mbalimbali.

Mabula alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wataalamu wa sekta ya ardhi katika Mkoa wa Mara akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya Serikali kupitia kodi ya pango la ardhi katika mkoa huo.

Alisema, baadhi ya halmashauri zimekuwa na kasi ndogo ya uandaaji hati za ardhi kwa kisingizio cha kuwa na wataalamu wachache wa kuandaa hati wakati halmashauri hizo zina wataalamu mbalimbali wa sekta hiyo na kutolea mfano wataalamu wa mipango miji, warasimu ramani, wapimaji na wathamani aliowaeleza wamekuwa wakisoma chuo kinachotoa taaluma ya sekta ya ardhi.

Aliongeza kuwa, iwapo watendaji wa sekta ya ardhi watafanya kazi kwa ushirikiano na kupeana malengo ya kuandaa hati, basi kasi ya utoaji hati itaongezeka na hivyo kuifanya wizara kuongeza makusanyo ya maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

"Ninyi nyote mmesoma katika chuo cha aina moja na mnazifahamu kazi za sekta ya ardhi mnaweza kupeana malengo na kila mmoja akashiriki kuandaa hati na inapofika hatua ya kukamilisha ndiyo apewe Ofisa Ardhi Mteule ili kukamilisha," alisema Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, kama watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri hawatakuwa wabunifu na kufanya kazi kwa kujiwekea malengo, kasi ya utoaji hati itakuwa ndogo na utaifanya wizara kutofikia malengo yake ikiwamo ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi ambayo kwa mwaka 2020/2021 ni Sh. bilioni 200.

Naibu Waziri alieleza kupitia kikao hicho kilichohudhuriwa pia na wakurugenzi wa Halmashauri za mkoa wa Mara kuwa wakati Serikali ikifikia nusu mwaka wa fedha 2020/2021 makusanyo ya kodi ya ardhi katika halmashauri nyingi yako chini ya asilimia, 50 jambo alilolieleza kuwa linatia shaka kama halmashauri hizo zitaweza kutimiza malengo katika muda uliosalia.

Mabula aliwaambia watendaji hao wa sekta ya ardhi kuwa katika robo ya mwaka wa fedha 2020/2021 anataka kuona halmashauri zote zinaongeza kasi ya makusanyo kwa kuhakikisha zinawabana wadaiwa sugu ili kulipa malimbikizo ya kodi ya ardhi na wale wadaiwa watakaokaidi kulipa basi wafikishwe kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba na Wilaya kwa hatua zaidi.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa Mara, Jerome Kiwia, alimueleza Mabula kuwa mkoa huo umeweza kukusanya takriban Sh. milioni 890.3 za kodi ya pango la ardhi, na kuwa, ofisi ya Ardhi katika mkoa huo imejiwekea mikakati ya kuhakikisha kasi ya makusanyo inaongezeka ikiwamo kusambaza ilani za madai kwa wadaiwa sugu na kutumia vyombo vya habari kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharibi Sospeter Magesse akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Dk. Joseph Chilongani, Meza, viti pamoja na madawati zaidi ya 200 vilivyotolewa na benki hiyo kwa shule za msingi na sekondari za Wilaya hiyo.**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wakuu wa shule wakabidhiwa madawati 1,000

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Filbeto Sanga, amewakabidhi walimu wakuu wa shule za sekondari wilayani humo madawati 1,000 ili kukabiliana na changamoto katika shule hizo.

Kukabidhiwa kwa madawati katika shule hizo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambalo linataka ifikapo mwishoni mwa Januari mwaka huu wanafunzi wote wawe wamekaa katika madawati.

Akikabidhi madawati hayo kwenye karakana zilizipo ofisini kwake, Sanga aliwataka wadau wa maendeleo ndani na nje ya Mkoa wa Pwani kuongeza nguvu ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa madawati inayochangiwa na ongezeko la wakazi wanaohamia na watoto kufuatia uwapo wa viwanda.

"Kwa sasa Mkuranga inakuwa na idadi kubwa ya wakazi wanaohamia kutoka maeneo mbalimbali, pia kuwapo kwa viwanda nako kunachangia wazazi kuja kufanya kazi... watato nao wanaongezeka katika shule, na hali hiyo inachangia hata madawati na madarasa kuongezwa," alisema.

Sanga aliwapongeza madiwani na wataalamu ambao wanaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mshamu Munde, kwa kutoa Sh. milioni 533, ili kuongeza nguvu katika ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari .

Pia Sanga aliwataka madiwa wawahamasishe wazazi na walezi kuwapeleka watoto shule, na watakaokaidi hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

# Kampuni ya madini yamwaga bil. 2.3/- kwa halmashauri

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

KAMPUNI ya uchimbaji wa madini ya Twiga Mineral, inayomiliki migodi ya Bulyanhuru na Buzwagi, imekabidhi Sh. bilioni 2.3 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Halmashauri ya Msalala ikiwa ni malipo ya ushuru wa huduma kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2020.

Fedha hizo zilikabidhiwa mwishoni mwa wiki kwa uongozi wa Wilaya ya Kahama na Meneja Mkuu Bulyanhuru na Buzwagi, Benedict Buzunzu.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema fedha hizo zitasaidia kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wananchi. Macha alisema fedha hizo ni sehemu ya mapato ya ndani ya halmashauri hizo, na kwamba zitaelekezwa kwenye kuboresha miundombini ya elimu na afya ambayo imekuwa na changamoto nyingi.

"Fedha hizi zikatumike kwenye mambo makubwa mawili tu, elimu na afya, mwenyekiti wataalamu wetu watakapoleta mapendekezo ya matumizi ya fedha hizi kwenye mabaraza yetu kwenye vipengere hivi hakikisheni mnapitisha kwa haraka " alisema Macha.

Aliongeza kuwa:"Hatuhitaji wanafunzi kila mwaka kuendelea kusubiria madarasa bali tunahitaji madarasa ndiyo yasubiri wanafunzi, aibu kubwa kila mwaka tunakumbushwa wajibu wetu wa ujenzi wa madarasa na viongozi wa juu wa serikali."

Aidha, Macha alisema upande wa Halmashauri ya Msalala kuna kata za Chela, Bulyanhuru, Mwalugulu na Bugalama, hivyo kunahitaji kukamilisha maboma ya madarasa yaliyojengwa na wananchi.

Katika Manispaa ya Kahama kwenye kata za Kagongwa, Busoka, Majengo na Mwendakulima pia watafanya hivyo.




Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, Benson Mihayo (wa pili kulia) akipokea mifuko 150 ya saruji kutoka kwa Meneja wa kiwanda cha bia (TBL) tawi la Mwanza, Godwin Fabian, ilizotolewa na kampuni kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa madarasa katika Kata ya Pasiasi. Kushoto ni Meneja Rasilimali watu wa TBL, Dora Nyambalya, Meneja Mawasiliano wa TBL Amanda Walter na Afisa Mtendaji wa Kata hiyo, Aloyce Mkono (kulia), jijini Mwanza mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi washauriwa kuomba zabuni kimtandao

**Na Joseph Mwendapole**

MAKANDARASI wametakiwa kuomba zabuni kwa kutumia mtandao wa kielektroniki kwani hivi sasa hakuna mkandarasi atakayepata kazi bila kuomba kupitia mfumo huo ulioanzishwa na serikali kwaajili ya maombi ya zabuni uitwao TANePS.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori, wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo yaliyoandaliwa na bodi hiyo jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yalihusu namna ya kusoma na kusaini mikataba ya kazi za ujenzi na namna makandarasi wanavyoweza kutumia mtandao wa kielekroniki kuomba zabuni mbalimbali za ujenzi. "Hivi sasa hakuna mkandarasi anaweza kupata kazi bila kuomba kupitia mfumo mpya wa mtandaoni hivyo kuna kila sababu ya kuujua mfumo na kuutumia na CRB imeona ni vyema ilete mafunzo haya kwa makandarasi wazalendo ili waujue na wautumie," alisema Nkori.

Makandarasi waliopata mafunzo hayo waliishukuru serikali kupitia bodi hiyo kwani mafunzo kama hayo yamekuwa yakiwaongezea thamani kwenye utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miradi mbalimbali.

Filomena Malenda kutoka kampuni ya Progressive women contractors Ltd, alisema mafunzo hayo yamewezesha kupata uelewa hasa juu ya mikataba ya kazi na hususani wanapopata changamoto kujua wapi wanaweza kukimbilia ili kupata msaada.

Idrisa Kinyagu aliishukuru CRB kwa mafunzo hayo ambayo alisema yamewasaidia kujua mambo mengi kama umuhimu wa bima na pia kuomba kazi kwa mfumo wa njia ya mtandaoni na namna ya kulinda mikataba

"Mafunzo haya yote yametupa uelewa sasa na kuhusu maombi njia mtandao kwa maana namna ya kutumia mfumo umeweza kurahisisha sana maombi mbalimbali hususani kwetu sisi makandarasi hivyo tunawashukuru sana Serikali na CRB," alisema Kinyagu.

## Rungwe wanalilia TARURA kero ya barabara

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa kitongoji cha Lumbila, Kijiji cha Kagwina Wilaya Rungwe, mkoani Mbeya, wameomba Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kuwajengea barabara ambayo imekuwa ikikwamisha biashara za mazao yao kufika sokoni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana na Nipashe, walisema ukosefu wa barabara kitongoji hicho kunasababisha wakate mawasaliano kati yao na vijiji vingine, hususan kipindi hiki cha mvua.

Mmoja wa wakazi wa kitongoji hicho, Matrida Chande alisema anaiomba serikali kuwakumbuka kwa kutengenezea barabara ambayo itarahisisha biashara ya mazao wanayouza ikiwamo kahawa, maparachichi na ndizi.

"Tunaomba serikali ituone, mimi ni mjane, hatuna barabara, tunalima sana kahawa, maparachichi, ndizi magari ya kubeba mizigo yanakataa kuja huku njia mbovu mazo yetu yanaoza hata mwaka jana yaliozea ndani," alisema Matrida.

Alisema mbali na hilo kuna uhaba wa maji na kufanya wakazi eneo hilo, kukosa huduma za kila siku za kibinadamu ikiwamo kuoga.

"Wakinamama tunalia machozi, tungefahamu anayehusika tungekufuata huko uliko, tunajitafutia shughuli lakini hakuna soko, tunabeba kiasi kidogo kichwani kufuata soko mbali," alisema Matrida.

Kisa Sakatali, alisema anashindwa kutembea umbali mrefu kufuata maji kwa sababu yeye ni mzee.

"Hapa nilipo natembelea fimbo, je, ndoo nitaweza kujitwisha. Kwenda hospitali nafikaje magari, pikipiki hazifiki. Tunaomba barabara wakazi wa kitongoji Lumbila," alisema Kisa.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Lumbila, Donald Majinja, alisema eneo hilo pamoja na kuwa maarufu katika kilimo cha mazao ya kibiashara ikiwamo kahawa, ndizi na maparachichi, ukosefu wa miundombinu ni kikwazo.

# Kijana matatani tuhuma za mauaji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, linamshikilia kijana mmoja mkazi wa Chimba Konde Wilaya ya Micheweni kwa tuhuma za mauaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alimtaja mtuhumiwa ni Huseein Haji Khamis (20).

Alieleza kuwa Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa raia mwema kuwa kuna mwendesha bodaboda ambaye anatambulika kwa jina la Seif Khamis (23) kuwa ana siku ya tatu hajulikani alipo na wala bodaboda yake.

Kamanda Sadi alieleza kwamba kuwa mtoa taarifa huyo aliliambia Jeshi la Polisi kuwa yeye na Seif (mwendesha bodaboda) walionana tangia Januari 23, mwaka huu na hadi juzi hajamuona na wala chombo chake hajakiona na hana taarifa zozote.

"Lakini alitupa taarifa kuwa alikuwa na ugomvi na kijana mmoja ambaye anaitwa Hussein (mtuhumiwa) kwa madai kuwa huyu Seif anamchukulia mkewe na alimsikia akimwambia kuwa atamfanyizia, hivyo inawezekana kuwa kweli ametimiza lengo lake," alisema Kamanda Sadi.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, Jeshi la Polisi lilifika katika Kijiji cha Jitenge ili kumfuata Hussein na hatimaye walifanikiwa kumtia mbaroni.

"Kwa bahati nzuri saa 8:15 za mchana tulimtia mbaroni mtuhumiwa na baada ya kufanyiwa mahojiano ya awali alikataa kuwa hana tatizo lolote na marehemu, lakini baada ya mahojiano zaidi alikiri kuwa wana ugomvi ila hajamfanyia chochote, ila baadaye alisema kuna shimo amemfukia mbwa," alieleza Kamanda Sadi.

Alieleza kuwa baada ya taarifa hiyo, polisi walikwenda hadi sehemu lilipokuwapo shimo anbalo Hussein alidai amemfukia mbwa na polisi walifukua shimo hilo, baada ya kufukua waliuona mwili wa Seif katika shimo hilo, huku miguu yake ikiwa imefungwa kamba.

"Hivyo polisi waliendelea kufukua hadi mwisho na hatimae walibaini aliyefukiwa ni Seif, na daktari baada ya kumfanyia vipimo aligundua alichomwa na kitu chenye ncha kali, huku mgongoni na usoni akiwa na mikwaruzo... baada ya hapo mwili ulikabidhiwa kwa jamaa zake kwa taratibu za mazishi," alisema Kamanda Sadi.

Kwa mujibu wa Kamanda Sadi, Jeshi la Polisi linaendelea kumshikilia kijana huyo na upelelezi utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa.

# TAKUKURU ilivyookoa mil. 500/- Kigoma

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma, imeingia makubaliano ya kurejesha vifaa vya umeme vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500 kutoka kampuni la JV State Grid Electrical and Technical Works Ltd kwa kushindwa kuvirejesha.

Ilishindwa kuvirejesha baada ya kumaliza mradi wa usambazi umeme vijijini (REA) awamu ya pili katika Mkoa wa Kigoma, uliotekelezwa katika wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko.

Akitoa taarifa ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba mwaka 2020, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, Stephen Mafipa, alisema kampuni hiyo baada ya kumaliza mradi mwaka 2016 walipaswa kurejesha vifaa hivyo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), lakini hawakutekeleza hadi TAKUKURU ilipoingilia kati kuchunguza. "Tusingeingilia kati vifaa hivi vilikuwa vimepotea, tumekubaliana ifikapo Februari 23, mwaka huu, vifaa hivyo virejeshwe TANESCO," alisema.

Pia Mafipa alieleza katika uchunguzi wa taarifa walizopewa, walifanikiwa kurejesha Sh. 94,665,946 ambapo kati ya fedha hizo, Sh. 27,665,000 zikiwa fedha za ada zilizolipwa na wananchi kwa ajili ya mafunzo ya usimamizi wa maduka ya dawa muhimu tangu mwaka 2015 ambayo hayakufanyika.

Fedha nyingine ni Sh. 23,350,000 zilizo kuwa zimelipwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) Kigoma kwa huduma hewa, Sh. 10,835,946 ya kodi ya mapato iliyokuwa imekwepwa kulipwa na Shule ya Sekondari ya Mwilan wilayani Kasulu na Sh. 54,000,000 alizodhulumiwa mwalimu mstaafu, Evodia Muliriye.

Raymond Antony, mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambaye ni mmiliki wa pikipiki, alisema TAKUKURU ifanye uchunguzi wa kina barabarani kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo.




Mshindi wa Tuzo za Ujasiriamali kwa Wanafunzi ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi kwa mwaka wa kwanza, Denis David, akizungmza na kutoa shukrani kwa waandaaji wa tuzo hizo baada ya kuibuka mshindi katika kilele cha mashindano hayo yaliyowakutanisha wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini, yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Denis David kaibuka mshindi kwa ubunifu wake wa kuhifadhi mazingira kwa kuokota Nywele katika saluni za vinyozi mbalimbali na kutengeneza Mbolea ya Maji pamoja na kutengenezea Viwatilifu vinavyouwa magugu mashambani, ambapo amejipatia kiasi cha dola za Kimarekazi 1000 (Elfu moja) zitakazomsaidia katika kuendeleza ubunifu wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yafunguka siri ya kupata faida ya bil. 205/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetangaza kupata faida ya Sh. bilioni 205.5 baada ya kodi kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2020 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 45.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema kuwa mafanikio hayo yametokana na utendaji imara uliojielekeza kukuza mapato na kuongeza ufanisi kwa kutumia teknolojia na kupunguza gharama za uendeshaji.

"Kwa miaka mitano iliyopita, Taifa lilishuhudia ukuaji endelevu wa uchumi uliochangiwa na sera makini za fedha na kodi. Ni kutokana na mazingira haya wezeshi pamoja na utekelezaji makini wa mpango mkakati wa benki tumefanikiwa kupata matokeo haya mazuri yaliyosaidia kukua kwa faida tuliyoipata," alisema.

Faida ya Benki kabla ya kodi iliongezeka kwa asilimia 40 kutoka Sh. bilioni 211.1 iliyopatikana mwaka 2019 mpaka Sh. bilioni 295.4 mwaka 2020, huku faida baada ya kodi nayo ikiongezeka kwa asilimia 45 kutoka Sh. bilioni 142.2 mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 205.5 mwaka 2020 na kufanya kuwa benki ya kwanza nchini kupata faida kubwa kiasi hicho.

Kwa mujibu wa Zaipuna, taarifa zake za fedha zisizokaguliwa pia zinaonyesha faida hiyo imechangiwa na ongezeko la mapato ya biashara yaliyopanda kwa asilimia 15 na udhibiti wa gharama za uendeshaji ambazo ziliongezeka kwa asilimia mbili tu ndani ya mwaka huo.

Kutokana na mpango mkakati wa benki wa kuongeza ufanisi wa utendaji na huduma za kijiditali, mapato mengine yaliongezeka kwa asilimia 19 kutoka Sh. bilioni 224.0 mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 266.2 mwaka 2020 yakichangiwa zaidi na ongezeko la wateja waliotumia huduma mtandaoni.

Alisema katika kipindi hicho, mapato yatokanayo na riba yaliongezeka kwa asilimia 13 kutoka Sh. bilioni 632.3 za mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 713.0 mwaka 2020.

Hata hivyo, lengo la mikopo chechefu liliongezeka kwa asilimia 19 kutoka Sh. bilioni 100.4 mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 119.3 mwaka 2020, mafanikio makubwa hasa ikizingatiwa changamoto kubwa iliyoletwa na janga la corona.

Alisema Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kama msimamizi wa sekta ya fedha, ilitekeleza wajibu wake vizuri kwa kutoa mwongozo uliotoa nafuu ya ukwasi hata kurekebisha urejeshaji wa mikopo iliyotolewa kwa wateja hasa waliopo kwenye sekta zilizoathirika zaidi na janga la corona.

HABARI KITAIFA

# Miaka 30 jela kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita mkoani humo, imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Nyanguku, Leonard Saidi (30), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kumpa ujauzito mwanafunzi mwenye umri wa miaka 18.

Binti huyo anasoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Nyanguku.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na vijana wengine wenye tabia ya kuwapa ujauzito wanafunzi kama yake.

Upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimpa ujauzito mwanafunzi huyo.

Aidha alisema mshtakiwa huyo alimtongoza mwanafunzi huyo ambaye jina lake tumelihifadhi na kufanya naye mapenzi kwa miezi miwili kisha akapata ujauzito.

Ilielezwa kuwa mama yake mzazi, Marieta Bupilipili alimgundua binti yake kuwa ni mjamzito, alikwenda kutoa taarifa polisi na shuleni. Hakimu alisema mwanafunzi huyo alipobanwa polisi, alimtaja mshtakiwa kuwa ni mpenzi wake na ndiye aliyempa mimba, mshtakiwa huyu alikamatwa na alipohojiwa alikiri kufanya mapenzi na mwanafunzi huyo.

Hakimu Maweda alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kulia), akimtunuku cheti Anna Shanalingigwa, mmoja wa wahitimu katika mahafali ya Programu ya Uanagenzi kwa Maofisa Watendaji Wakuu (CEO Apprenticeship Program). Kushoto ni Sanjay Rughani, Mwenyekiti wa Jukwaa la Taasisi ya Wakurugenzi na wamiliki wa kampuni binafsi (CEOrt). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Majaliwa aipa CEOrt mbinu za kupata watendaji wakuu wazawa

**NA MWANDISHI WETU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa wito kwa Jukwaa la Taasisi ya Wakurugenzi na wamiliki wa kampuni binafsi (CEOrt) kushirikiana na serikali na taasisi nyingine ili kubaini maeneo yenye uhitaji wa viongozi wakuu wazawa na kutoa mafunzo yenye tija.

Pia ameitaka Bodi ya wakurugenzi wa Jukwaa hilo kuandaa mipango ya mafunzo yenye lengo la kutambua na kujenga uwezo kwa Watanzania katika sekta za kipaumbele hususan sekta ya madini, mafuta na gesi, ujenzi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Majaliwa alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika mahafali ya wahitimu wa Programu ya Uanagenzi kwa Maofisa Watendaji Wakuu (CEO Apprenticeship Program).

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Chuo cha Strathmore Business School (SBS) cha Kenya, jumla ya washiriki 16 walihitimu mafunzo hayo yaliyokuwa yameandaliwa na CEOrt kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi,Vijana na Ajira).

Mafunzo hayo yamelenga kuwawezesha Watanzania kushika nyadhifa za juu za Uafisa Mtendaji Mkuu (CEOs) na Ukurugenzi Mtendaji (MDs) katika makampuni na taasisi mbalimbali.

Waziri Mkuu alisema ushirikiano wa CEOrt na Taasisi ya Uongozi inayoendesha programu za mafunzo ya uongozi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Alto cha Finland, utaleta tija, kuondoa marudio na kuimarisha ubunifu katika kutoa mafunzo na kuleta manufaa kwa washiriki wa mafunzo hayo.

Pia, Waziri Mkuu aliwataka CEOrt washirikiane katika kuwajengea uwezo wa wataalamu wabobezi katika masuala ya uendeshaji wa miradi mikubwa ya kimkakati.

"Mafunzo haya yamekuja wakati muafaka kwani yanaendana na falsafa ya Serikali ya awamu ya tano ya 'hapa kazi tu', pia yamekuja katika kipindi ambacho nchi imeingia katika uchumi wa kati hivyo viongozi hao watumie ujuzi na weledi katika maeneo ya usimamizi wa rasilimali watu, rasilimali fedha na miradi," alisema.

Aidha, akizungumza katika mahafali hayo, Mwenyekiti wa CEOrt, Sanjay Rughani, alisema mafunzo hayo pia yamelenga kuwajengea wataalam wa kitanzania uwezo mkubwa ili waweze kushindana katika kuhudumu kwenye nafasi za utendaji mkuu katika taasisi, programu na miradi mikubwa ya kitaifa na kimataifa.

Alisema programu hiyo ilianza miaka miwili na nusu iliyopita, baada ya kufanya utafiti na kubaini kuwa asilimia 60 ya viongozi wa kampuni mbalimbali wenyewe walitaka watanzania na waafrika wamiliki hizi nafasi za mkurugenzi mtendaji lakini kuwapata hawa Ma-CEOs ilikuwa kazi ngumu sana.

"Katika programu hii washiriki 16 ambao wamehitimu, wametoka kwenye kazi zao kama za ofisa rasilimali watu na nyingine lakini watatu kati yao wamepandishwa cheo na kuwa Ma-CEOs katika makampuni ya Songas, PASS na Access Benki.

"Kwa kweli nina furaha kubwa kwani nilikaa nao tangu siku ya kwanza ya mafunzo na sasa wanaweza kuzungumza mambo ya kidunia, kisera, kiuchumi na kuwezesha kampuni kupiga hatua," alisema.

# Vijana watakiwa kutumia fursa za kimitandao

**Na Anaeli Mbise**

VIJANA wametakiwa kutumia vizuri majukwaa ya kimitandao ambayo yanatoa fursa mbalimbali za kujipatia kipato kutokana na kazi zinazopatikana kwenye majukwaa hayo.

Ofisa Mtendaji Mkuu na mbunifu wa jukwaa la Gigspace, Ashura Babi, akiwa na mwanzilishi mwenza, Steve Mawalla, wamesema waliamua kuanzisha jukwaa hilo kwa ajili ya kuwaongezea na kuwafungulia vijana pamoja na wafanyakazi fursa pia za ajira kupitia mtandaoni.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe, Ashura, alisema waliona changamoto za watu kupata ajira baada ya kuhitimu masomo inakuwa kubwa, hivyo wakaamua kuanzisha jukwaa hilo ambalo linakuwa linaunganisha mfanyakazi na kampuni binafsi.

"Lengo kuu la jukwaa ni kuunganisha mfanyakazi ambaye ana kazi, ila anakuwa anafanya kazi akiwa huru mtandaoni pamoja na wale ambao hawana ajira wanajisajili kwa fani zao na tunawaunganisha na kampuni za kibiashara na wanatimiza malengo ya maisha yao kwa kujisajili kupitia tovuti ya Gigspace," alisema Ashura.

Ofisa huyo alisema kuwa kwa kutumia mtandao huo, kampuni nyingi ambazo zitakuwa zinafanya kazi ndani ya jukwaa hilo zitakuwa zinalipa kodi ya serikali kwa makato ambayo ni nafuu, lakini pia ulipwaji wa wafanyakazi unakuwa ni wa kiwango ambacho siyo umiza kwa kampuni za biashara na wafanyakazi hao.

Steve Mawalla, muanzilishi mwenza wa jukwaa hilo, alisema kuwa watu wengi wanaingia mtandaoni kutafuta taarifa ambazo hazina tija na manufaa kwao, lakini kupitia jukwaa hilo wakiingia watapata taarifa ambazo zitawasaidia na kutumia fursa zilipo.

Nipashe
Spotika



WANASOKA NYOTA 10 WENYE WAFUASI WENGI INSTAGRAM UK. 12-13



# WACHEZAJI WA5 WANAOSUBIRI MBELEKO YA TUCHEL CHELSEA

## ISIKUPITE

MATOKEO ya sare tasa juzi kwenye Ligi Kuu England, yanaifanya Arsenal kuendelea kushikilia rekodi ya kutofungwa katika mechi sita zilizopita za ligi dhidi ya Manchester United, tangu ilipopoteza ugenini msimu wa 2017-18. Hiyo ni rekodi ndefu zaidi kwa 'Gunners' ya kutofungwa dhidi ya 'Mashetani Wekundu' hao kwenye ligi tangu Oktoba 1980 hadi Mei 1983.



**LONDON,** England

MASHABIKI wa Chelsea tayari wameachana na Frank Lampard baada ya miezi 18 ya kuwa kocha wa 'Blues' hao.

Lampard alikuwa kwenye presha kubwa kwenye kikosi chake hicho, akichukua Chelsea ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo. The Blues hao walikuwa na mwanzo mzuri wa msimu huu wakati walipocheza mech 17 bila kufungwa. Hata hivyo, mambo yakabadilika na kila kitu kikawa tofauti.

Mchezaji huyo wa zamani wa Blues aliichukua klabu hiyo kabla ya msimu uliopita. Klabu hiyo ilikuwa kwenye kufungiwa kutofanya usajili baada ya kumpoteza Eden Hazard kwenda Real Madrid. Hata hivyo, Lampard akajaribu kulibeba jahazi.

Aliwapa nafasi wachezaji wengi kuchomoza katika kikosi cha kwanza kama Reece James, Mason Mount, Tammy Abraham na Billy Gilmour ili kujiimarisha wenyewe kwenye kikosi cha kwanza.

Hata hivyo, matokeo yamekuwa tofauti kabisa msimu huu baada ya kutumia pauni milioni 200 kwa kusajili wachezaji wapya. Thomas Tuchel amechukua mikoba ya kuinoa timu hiyo. Mjerumani huyo naye alifukuzwa kule Paris Saint-Germain mapema mwezi uliopita.

Ujio wa kocha mpya mara zote unaleta mambo yasiyotabirika. Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kuimariika chini ya kocha huyo mpya, Tuchel...

### #5. TIMO WERNER

Kama kuna mchezaji alikuwa akihitaji mabadiliko hayo ni Timo Werner. Mjerumani huyo alitua Chelsea akiwa na heshima kubwa kama mmoja wa mastraika bora duniani.

Lakini mshambuliaji huyo mambo yakamwendea kombo kwani kiwango chake kilishuka ghafla. Mjerumani huyu amefunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho tano msimu huu, lakini kuna hisia kwamba anaweza kufanya vizuri zaidi. Lampard alikuwa akishutumiwa namna alivyokuwa akimtumia Werner kwenye timu yake.

Tuchel anajua uwezo wa Werner tangu wakiwa pamoja kule kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

### #4. CHRISTIAN PULISIC

Christian Pulisic hatimaye alijiunga na Chelsea kabla ya kuanza kwa msimu uliopita. Winga huyu alikuwa na wakati mgumu Chelsea huku akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na kuzoea soka la Uingereza.

Hata hivyo, winga huyo sasa ameweza kukabiliana na majeraha na alimaliza msimu uliopita akiwa imara. Alifunga mabao 10 kwa jina lake, bahati mbaya akaumia tena wakati wa mchezo wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Arsenal.

Pulisic alianza msimu huu akiwa majeruhi, lakini kulikuwa na matumaini kwamba anaweza kupona katikati ya msimu. Thomas Tuchel alifanya kazi na Pulisic kule Dortmund. Winga huyo aliwahi kubainisha kwamba, Tuchel alimsaidia yeye kuimarika. Tuchel anajua kuimarisha wachezaji na Blues hao wana imani kubwa naye.

### #3. JORGINHO

Jorginho ni mmoja wa wachezaji aliyetumiwa sana na Frank Lampard msimu uliopita. Hiyo ni kutokana na majeruhi ya N'Golo Kante, Jorginho alicheza kama nguzo muhimu kwenye nafasi ya kiungo Chelsea wakati wa msimu wa kwanza chini ya Lampard klabuni hapo. Lakini baadaye Lampard alihamia kwa Billy Gilmour.

Msimu huu Jorginho alianza kucheza mara kwa mara, huku baadhi ya mechi akicheza vibaya.

Ujio wa Tuchel unaweza kuwa na matokeo chanya sana kwa Jorginho. Mjerumani huyo anapenda kumchezesha kiungo anaeondosha mpira haraka.

### #2. ANTONIO RÜDIGER

Antonio Rüdiger ni mmoja wa wachezaji wachache wa Chelsea ambao walikuwa na nafasi ngumu kuaminiwa na Frank Lampard msimu uliopita. Licha ya kuwa mlinzi ghali zaidi baada ya Thiago Silva klabuni hapo, alikosa namba mbele ya Kurt Zouma.

Alitaka kuondoka misimu miwili iliyopita baada ya kupona majeraha ya goti. Lakini ilishindikana kutokana na kiwango kibovu. Lakini sasa mlinzi huyo ana matumaini mambo yanaweza kuwa tofauti sasa. Kuwasili kwa Tuchel kutamuunganisha na mlinzi huyo wa kati wa Ujerumani. Kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain awali alionyesha nia ya kutaka kumsajili Rüdiger, Hiyo maana yake ni kwamba, wawili hao wanaweza kufanya kazi vizuri kwa pamoja.

### #1. KAI HAVERTZ

Chelsea ilivunja rekodi yao ya usajili kwa kumsajili, Kai Havertz kipindi cha majira ya joto kilichopita. Raia huyo wa Ujerumani alikwenda London alikuwa na matumaini mengi ya kung'ara.

Hata hivyo, mambo hayakwenda kama yalivyopangwa. Mjerumani huyo amefunga bao moja tu la ligi msimu huu. Kuzoea ligi mpya kunamuweka kwenye wakati mgumu Havertz .

Hata hivyo, Frank Lampard alimtumia Havertz katika sehemu nyingi tofauti, lakini hazikuzaa matunda. Kuna wakati Lampard aikuwa akimchezesha Mjerumani huyo kama winga lakini wapi.

Thomas Tuchel anajulikana kama mmoja wa makocha wenye mbinu nyingi sana. Anaweza kumuimarisha na kumuweka pale anapostahili..

## Extra Time

# WANASOKA NYOTA 10 WENYE WAFUASI WENGI INSTAGRAM



RONALDO

**LONDON,** England

MITANDAO ya kijamii imekuwa na nguvu kubwa zaidi kwenye jamiii kwa sasa, hasa kutokana na upatikanaji rahisi wa 'intaneti'. Mitandao hiyo imekuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya watu na imekuwa na umaarufu mkubwa sana duniani.

**Mtandano wa kijamii wa Instagram haraka sana ndio umekuwa kama unaokimbiliwa zaidi na mastaa wakubwa duniani na wengi wao wanatumia huko kama kutoa taarifa zao mbalimbali.**

Katika makala haya, tunawaangalia wachezaji soka 10 ambao wana wafuasi wengine zaidi kwenye mtandano wa Instagram kwa sasa. Takwimu hizi zimechukuliwa hadi mwishoni mwa mwaka 2020, twende sasa...

### #10. SERGIO RAMOS (REAL MADRID, HISPANIA)

Idadi ya wafuasi wake wa Instragram (mwishoni mwa mwaka 2020): Mil. 42.5

Sergio Ramos ni mmoja wa wachezaji maarufu duniani kwa sasa. Nahodha huyu wa Real Madrid na Hispania amejiimarisha yeye mwenyewe kama mlinzi bora katika kizazi chache, wakati akisaidia mashambulizi ya mara kwa mara kuliko beki yoyote.

Anashikilia rekodi kadha za klabu na kitaifa, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, anacheza katika msimu wake wa 16 akiwa pale Real Madrid na amewasaidia 'Los Blancos' hao kushinda mataji 22 yakiwemo matano ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ramos ameichezea Hispania tangu mwaka 2005, akishikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi kama mchezaji (178). Ameshinda taji la Dunia na mawili ya Ulaya.

### #9. PAUL POGBA (MANCHESTER UNITED, UFARANSA)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 42.6

Paul Pogba anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora kabisa duniani. Ana kipaji chake anakiendeleza katika umri wake wa miaka 27 akishikilia rekodi ya kuwa mchezaji ghali kwenye Ligi Kuu England wakati aliponunuliwa na Manchester United kwa pauni milioni 105.

Pogba ameichezea Ufaransa mechi 75 na alikuwa nguzo muhimu wakati wakishinda Kombe la Dunia mwaka 2018 na Ufaransa.

### #8. GARETH BALE (TOTTENHAM HOTSPUR, WALES)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 43.7

Anayetaka kuondoka Real Madrid, Gareth Bale, kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Tottenham Hotspur. Huku akiwa amekosa nafasi kule Madrid, bado anachukuliwa kama mchezaji muhimu duniani.

Baada ya kuchomoza kutoka Tottenham Hotspur akiwa kinda, alihamia Real Madrid mwaka 2013 ambako alipata mafanikio makubwa. Kuna kipindi bila shaka yoyote, Bale alikuwa miongoni mwa wachezaji watano bora zaidi duniani na akatumia muda wake mwingi kuwaadabisha wapinzani.

Katika miaka yake saba aliyokaa pale Madrid, ameisaidia kutwaa mara nne taji a Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga mara mblili, kati ya jumla ya mataji 13 aliyoshinda.

Bale amekuwa pia mchezaji muhimu kwa Wales, na ametajwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa nchini hiyo mara sita.

### #7. KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN, UFARANSA)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 45.8

Unajua namna gani wachezaji wanavyokuwa maalumu sana wakati wanapokuwa bora katika umri wa miaka 22. Kumekuwa hakuna shaka juu ya kiwango cha Kylian Mbappe.

Licha ya umri wake, Mbappe amecheza jumla ya mechi 204 kwa ngazi ya klabu na kufunga mabao 131 na kutoa pasi za mwisho 74. Kwa sasa anacheza msimu wake wa nne akiwa na Paris Saint-Germain, na tayari amefunga mabao manne.

Straika huyo aliiwakilisha Ufaransa kwenye Kombe la Dunia na kubeba taji. Mbappe alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga bao kwenye mashindao hayo na akapata tuzo ya mchezaji bora kijana.

### #6. ZLATAN IBRAHIMOVIC (AC MILAN, SWEDEN)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 46.0

Baada ya kujitambulisha mwenyewe kwenye dunia ya soka, Zlatan ameendelea kuwa kwenye ubora ule ule licha ya kwamba sasa yeye ni gwiji.

Straika huyo wa Sweden ni mmoja wa washambuliaji bora duniani kwa sasa. Ukiwatoa Cristiano Ronaldo na Lionel Messi hakuna mchezaji mwingine aliyefunga mabao mengi zaidi kama Ibrahimovic.

Kipindi chake cha uchezaji amekipiga Barcelona, Manchester United, PSG, Juventus, Inter na AC Milan. Na amebeba zaidi ya mataji 30.

Ameichezea Sweden katika michuano ya kimataifa kwa miaka 16 kabla ya kutangaza kustaafu mwaka 2016.

### #5. MARCELO (REAL MADRID, BRAZIL)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 46.1

Wakati akijatwa kama mmoja wa walinzi wa kushoto bora zaidi kwenye historia ya soka, Marcelo alicheza soka Real Madrid na timu ya Taifa ya Brazil.

Kwa sasa yupo kwenye msimu wake wa 15 na Real Madrid, Marcelo ameshaonyesha ugwiji wake kwa kushinda mataji 22 akiwa na Los Blancos hao. Yakiwamo matano ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amecheza jumla ya mechi 58 kwa Brazil.

### #4. JAMES RODRIGUEZ (EVERTON, COLOMBIA)

Idadi ya mashabiki wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 46.6

James Rodriguez alijitangaza kwenye ulimwengu wa soka katika fainali za Kombe la Dunia mwaka 2014 wakati alipofunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi tano na akatwaa Kiatu cha Dhahabu. Tangu hapo raia huyo wa Colombia akaichezea Real Madrid, Bayern Munich na Everton.

### #3. NEYMAR (PARIS SAINT-GERMAIN, BRAZIL)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 144

Neymar bila shaka yoyote ni mmoja wachezaji bora zaidi karika kizazi chake.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, ni mmoja wa wanamicheo wenye soko kubwa zaidi nje na ndani ya uwanja. Na ndio maana yeye ni miongoni mwa wanasoka watatu tu wenye wafuasi zaidi ya 100 kwenye Instagram.

Raia huyo wa Brazil ameshinda mataji kadhaa na Barcelona na PSG - baada ya kutua hapo akitokea Barcelona.

### #2. LIONEL MESSI (BARCELONA, ARGENTINA)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 174

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi dunia kuwahi kushuhudiwa, Lionel Messi ni miongoni mwa wenye wafuasi wengi zaidi Instagram.

Messi mwenye umri wa miaka 33 kwa sasa, anacheza katika msimu wake wa 17 pale Barcelona, ambako kwa sasa ni nahodha na ameshinda jumla ya mataji 33, yakiwamo 10 ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #1. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS, URENOL)

Idadi ya wafuasi wa Instagram (mwishoni mwa 2020): Mil. 250

Nyota huyo wa Ureno ni mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani na kwenye suala la masoko yupo vizuri sana.

Ndio maana yeye ndiye mwanasoka pekee mwenye wafuasi wengine zaidi kwenye mtandano wa Instagram.

## Nukuu

"Ni vigumu kwangu kuweka kwa maneno upendo ninaohisi kwa klabu na mashabiki [wa Arsenal], ninawezaje kuelezea miaka minane ya shukrani kwa barua moja? Nitakuwa Arsenal kwa maisha yote bila shaka juu ya hilo," **aliyekuwa kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil, akitoa hisia zake kwa klabu hiyo kwa njia ya barua pepe kabla ya kujiunga rasmi na Fenerbahce ya Uturuki.**



"Kwa muda mrefu nimekuwa ndani ya Chelsea ila ninafurahi kufanya kazi hapo, ninapenda kuwashukuru mashabiki kwa sapoti ambayo wamenipa kwa miezi 18, uongozi pia na wote ambao wamekuwa pamoja nami. Ninajua changamoto ni jambo ambalo haliepukiki, ila kwa kushindwa kufikia mafanikio kwangu ni maumivu, ninaushukuru uongozi kwa ujumla na kila mmoja, nawatakia mafanikio mema," **aliyekuwa Kocha wa Chelsea, Frank Lampard baada ya kufutwa kazi.**



"Nimehuzunishwa kwa kushindwa kwao kumpa muda wa kutosha afanye mengi mazuri yenye mafanikio, siku zote sifurahii mwenzangu kupoteza kazi. Frank [Lampard] si tu nimewahi kufanya naye kazi, bali ni mtu muhimu kwenye kazi yangu, kwa hiyo namuonea huruma kufukuzwa kwake," **Kocha wa Tottenham, Jose Mourinho, akimlilia Lampard kutimuliwa Chelsea.**



Nipashe **Spotika**



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini juzi kujiandaa na Ligi Kuu Bara pamoja michuano ya Simba Super Cup iliyofikia kileleni jana. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, NAMUNGO NA VIPORO VIGUMU KULIKA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KINYANG'ANYIRO cha Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajiwa kuendelea tena Alhamisi wiki hii kwa mechi za viporo zinazozihusu timu za Simba na Namungo zilizokuwa na jukumu la kuiwakilisha nchi kwenye mechi za kimataifa.

Simba ilikuwa kwenye mtihani wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi, huku Namungo ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF) na ikafanikiwa kutinga raundi ya pili na sasa inatarajiwa kucheza mechi ya mtoano dhidi ya CD Primeiro de Agosto ya Angola kutafuta timu itakayotinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

**Kutokana na kazi waliokuwa nayo wawakilishi hao, Bodi ya Ligi ikiahirisha baadhi ya mechi zao na sasa zinakwenda kupigwa kuanzia Alhamisi, Februari 4 na Jumapili, Februari 7, wiki hii.**

Mara ya mwisho kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilichezwa Januari 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Gwambina, kati ya wamiliki wa uwanja huo, timu ya Gwambina FC dhidi ya timu ngumu ya Biashara United ya mkoani Mara, wenyeji wakipoteza kwa bao 1-0.

Tayari Bodi ya Ligi (TPLB) imeweka wazi ratiba ya viporo hivyo ambavyo vinaonekana kuwa si vya kitoto kwa timu zote zitakazocheza, hapa tunazitazama...

### #1. DODOMA JIJI VS SIMBA (FEBRUARI 4)

Itakuwa ni mara ya kwanza kwa timu hizo mbili kukutana katika historia ya soka nchini. Dodoma Jiji imepanda msimu huu, hivyo itaonja ladha halisi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kucheza na mabingwa wa soka siku hiyo ya Februari 4, Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Ni mechi ambayo Dodoma Jiji itabidi iwe makini, kwani pamoja na kwamba inacheza kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri Dodoma, lakini ikumbukwe kuwa ni uwanja huo huo ambao wenzao wanaoutumia uwanja huo, JKT Tanzania ilikutana na kipigo cha paka mwizi cha mabao 4-0.

Pia ni mechi ambayo ni kipimo cha kwanza cha kocha mpya Mfaransa, Didier Gomes Da Rosa kwenye Ligi Kuu. Vile vile Simba itakuwa na wachezaji wapya ambao huenda wakaonekana kwa mara ya kwanza wakicheza Ligi Kuu kama Perfect Chikwende, Allan Lwanga, na wengineo.

### #2. KMC VS NAMUNGO (FEBRUARI 4)

Ni mechi ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam siku ya Alhamisi, Februari 4. Itazikutanisha timu ambazo moja inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa msimu huu, nyingine iliiwakilisha nchi msimu uliopita. Zote ziliwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

KMC, ambayo kwa sasa inakamata nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi kwa pointi 22, ilicheza Kombe la Shirikisho msimu uliopita, huku Namungo ambayo mpaka sasa ipo kwenye michuano hiyo, lakini kwenye ligi inashika nafasi ya 15 na pointi 18 ilizonazo.

### #3. SIMBA VS AZAM FC (FEBRUARI 7)

Hii ni mechi ya kukata na shoka, kwani itazikutanisha timu ambazo zote zipo kwenye mchuano mkali wa kuusaka ubingwa.

Kama vile haitoshi itakuwa ni mechi ya kisasi kwa Azam, kwani msimu uliopita iligeuka kuwa kibonde kwa Simba, ikifungwa mechi zote ambazo imekutana nayo. Ilichapwa bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza Ligi Kuu Bara, na kisha Simba ikashinda tena kwa mabao 3-2 mechi ya mzunguko wa pili.

Zilipokutana kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, Simba ilishinda mabao 2-0 na kusonga mbele hadi kwenda kutwaa kombe hilo. Mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikiwa mwenyeji, kila timu ikiwa na kocha mpya.

Wakati Simba itakuwa na Didier, Azam FC itakuwa chini ya George Lwandamina. Lakini pia wakati Simba itakuwa na baadhi ya wachezaji wapya, akiwamo Chikwende, Azam itakuwa na Prince Dube ambaye tayari amepona na yuko fiti, golini huenda akakaa kipa mpya, Mganda Mathias Kigonya.

### #4. NAMUNGO VS RUVU SHOOTING (FEBRUARI 7)

Kwenye mechi hii, Namungo itakuwa inarejea nyumbani kwenye Uwanja wa Majaliwa kwa mara ya kwanza tangu Desemba 9, mwaka jana, ilipocheza dhidi ya Biashara na kutoka suluhu bila kufungana.

Baada ya hapo ilikuwa ikicheza mechi ugenini, lakini pia hata mechi za kimataifa ilikuwa ikicheza kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi, kabla ya kwenda Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Itakuwa ni mechi itakayosubiriwa mno na mashabiki wa mkoa wa Lindi ambao hawajaona timu yao kwa muda mrefu, hivyo kutarajia kujaza uwanja kwa ajili ya kuipongeza kwa kufanikiwa kusonga mbele kwenye mechi za kimataifa na wachezaji watakuwa na jukumu la kuwapatia zawadi ya ushindi dhidi ya Ruvu Shooting.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER United imeshindwa kufunga bao katika mechi tatu mfululizo za ligi dhidi ya Arsenal kwa mara ya kwanza tangu katikati ya Septemba 1981 na Mei 1983 (wakiwa wamekutana mara nne kipindi hicho). Lakini pia sare tasa waliyoipata juzi kwenye Ligi Kuu England ni ya kwanza dhidi yao tangu Februari 2014.



## HABARI DODOMA

# IJA yakamilisha mtaala mafunzo kwa mawakili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), kimekamilisha kutengeneza mtaala wa mafunzo elekezi kwa mawakili na wanasheria wapya wa sekta ya umma, ili kujua mifumo ya uendeshaji wa shughuli za kiserikali.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye maonyesho ya Wiki ya Sheria na maadhimisho ya miaka 100 ya Mahakama, Mhadhiri wa Chuo hicho, Philemon Raulencio, alisema mafunzo hayo yamelenga katika kuwajengea uwezo waajiriwa wapya wa kada ya sheria wa taasisi, wizara, idara, wakala na mamlaka za serikali.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanajua mifumo ya uendeshaji wa shughuli za kiserikali, uongozi na utumishi wa umma ili kuwa na utumishi ulio bora.

Mhadhiri huyo alisema mtaala huo umekamilika na ulishirikisha wadau wa sheria wakati wa kuuandaa na kuwa kwa sasa chuo kinasubiri mwitikio wa watumishi.

"Tunataka wajue na waive katika kutunza siri za serikali na nidhamu na maadili ya utumishi wa umma na pia wajue kuwa wanatakiwa kuutumikia umma wa Watanzania katika taasisi yake," alisema.

Alitoa rai kwa taasisi, wizara, idara, wakala na mamlaka za serikali kuhakikisha watumishi wao wa kada ya sheria wanapata mafunzo hayo.

"Mafunzo haya si lazima kwenda Lushoto, kama taasisi itaona tutoe mafunzo katika ofisi zao tunaenda kufanya hivyo, kwa kuwa Waraka namba tano wa mwaka 2011 wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaelekeza kutolewa kwa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya katika utumishi wa umma,"alisema.

Alibainisha kuwa Chuo hicho kimekasimiwa madaraka ya kuandaa na kutoa mafunzo ya awali na elekezi kwa waajiriwa wote wa kada ya sheria katika sekta ya umma nchini.

Kuhusu programu ya kutoa mafunzo kwa madalali na wasambaza nyaraka wa mahakama, Raulencio alisema ndani ya miaka mitatu tangu kuanza programu hiyo watu 289 wamehitimu mafunzo hayo.

# Waziri, wazalishaji wa sukari wajadili kuongeza uzalishaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amefanya mzungumzo na wazalishaji wa sukari nchini ili kutatua kero zinazowakabili na kuongeza uzalishaji.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wazalishaji hao, Waziri Mwambe alisema serikali inalenga kuongeza uzalishaji wenye tija kwa kutumia teknolojia na miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji.

"Tunataka sukari ipatikane kwa urahisi wakati wote nchini.Leo nimekutana na nyie kwa lengo la kujifunza na kujua kero mlizonazo katika uzalishaji wa sukari nchini, nawaahidi tutazifanyia kazi," alisema.

Aliwatoa wasiwasi wazalishaji hao kuwa Serikali itahakikisha inashughulikia kero zao ili kuongeza uzalishaji zaidi nchini.

Wiki iliyopita, Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, alitaja maeneo sita nchini yanayofaa kwa uwekezaji kilimo cha miwa, yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 976,000 za sukari kwamwaka.

Alitaja maeneo hayo ambayo ukubwa wake upo kwenye mabano kuwa ni Kibondo (hekta 25,000), Kasulu (hekta 37,000), Rufiji (hekta 25,000), Songwe (hekta 22,000), Mara (hekta 12,000), Mpanda (hekta 27,462), na Rukwa (hekta 12,372).

"Serikali kupitia Bodi ya Sukari na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) itaendelea kutangaza maeneo haya kwa ajili ya kupata wawekezaji na kuongeza uzalishaji wa sukari nchini," alisema.

Pamoja na hayo, alisema mahitaji ya sukari yanaongezeka na kwamba serikali imeweka mikakati ya kuongeza uzalishaji ambapo inaendelea kufuatilia mipango ya upanuzi wa viwanda vya Kilombero, Kagera na Mtibwa vinavyotarajiwa kuzalisha tani 519,000 ifikapo mwaka 2024/25.

"Hivyo ukamilishaji wa viwanda hivi na mchango wa uzalishaji kutoka miradi mipya ya Bagamoyo na Mkulazi kiasi cha sukari tani 704,000 kinatarajiwa kuzalishwa katika kipindi hicho," alisema.

Alibainisha kuwa mahitaji ya sukari yatakuwa yameongezeka hadi tani 568,371 katika kipindi hicho na kiasi cha tani kitakachozalishwa tani 704,000 kitatosheleza mahitaji hayo na kuwa na ziada ya tani 135,629.

Awali, alisema kama eneo lote la mashamba ya miwa lenye hekta 57,640 lingevunwa jumla ya tani Milioni 4.01 za miwa zingepatikana na kuzalisha sukari tani 401,072 kwa mwaka.

Alisema uzalishaji wa sukari kwa mwaka hapa nchini ni wastani wa tani 300,000 ambapo katika msimu wa mwaka 2020/21 jumla ya tani 377,527 za sukari zitazalishwa kutoka kwenye viwanda vilivyopo vya Kilombero Sugar Company Ltd, Mtibwa Sugar Estate, Kagera Sugar Ltd, TPC Ltd na Manyara Sugar Ltd.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ,Prof .Palamagamba Kabudi (kushoto) akipokea baadhi ya vitabu na machapisho kutoka kwa Mhadhiri Chuo cha Mahakama Lushoto,Philemon Raulencco alipotembelea bada la Chuo hicho mwisho wa wiki kwenye maonesho ya wiki ya sheria yanayoendelea Jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Marufuku wakulima wa tumbaku kukata magogo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Tumbaku imepiga marufuku wakulima kukata magogo kwa ajili ya kukaushia tumbaku badala yake wametakiwa kutumia majiko sanifu yanayotumia matawi.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Stanley Mnozya, alisema matumizi ya magogo yanasababisha kukata miti ovyo na kuharibu mazingira, hivyo wakulima wanapaswa kutumia majiko hayo.

Aidha, alisema matumizi ya mabani ya kizamani ambayo hutumia kuni nyingi yamepungua kutoka 137,139 msimu 2015/2016 hadi 60,065 msimu 2019/2020.

"Kupungua huku kwa mabani ya kizamani kumewezesha kupungua kwa kiasi kikubwa cha matumizi ya kuni za kukaushia tumbaku, kuongeza ubora na kurahisisha kazi kwa mkulima," alisema.

Alisema hatua hiyo imeongeza ubora wa tumbaku na kurahisisha kazi kwa mkulima.

Kadhalika, alisema mabani ya kisasa na yaliyoboreshwa yameongezeka kutoka asilimia 39 msimu 2015/2016 hadi asilimia 68 msimu 2019/2020,lengo ikiwa ni kuhakikisha wanafikia asilimia 100 msimu 2020/2021.

Kuhusu upandaji miti kwenye mashamba yanayolima tumbaku, Mnozya alisema mwitikio wa wakulima kupanda miti umeongezeka kutoka asilimia 73 ya lengo la msimu 2015/2016 hadi kufikia asilimia 90 katika msimu wa 2019/2020.

"Miti iliyopandwa imestawi kutoka asilimia 56 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 61 katika msimu wa 2019/2020," alisema.

Alisema Bodi hiyo itaendelea kuwafikia wakulima na kutoa elimu ili kuwa na tumbaku bora inayokidhi soko la ushindani.

"Bodi inafanya jitihada za kuhakikisha wanasonga mbele katika uendeshaji wa zao hili, hivyo wakulima wasiwe na wasiwasi wajiandae kwa ajili ya msimu ujao," alisema Mnozya.

Pia alisema Bodi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku (TORITA), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), Wizara ya Kilimo na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ilifanya ziara China kutafuta masoko ya tumbaku.

# Wataka klabu za upandaji miti shuleni

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI za Miji, Wilaya na majiji nchini, zimeshauriwa kuanzisha klabu za upandaji miti kwenye jamii hasa kwenye shule za sekondari na vyuo ili kuwajengea vijana utamaduni wa kupanda miti ili kuongeza ufanisi wa utunzaji wa mazingira.


Ushauri huo ulitolewa na wadau wa mazingira wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miti wilayani Rungwe ambalo lilifanyika katika chanzo cha maji cha Msasani mjini Tukuyu.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Rungwe, John Boya, alisema baadhi ya wananchi hawana utamaduni wa kupanda miti kwa sababu hawakujengwa tangu wakiwa wadogo.

Alisema pamoja na kuanzisha klabu hizo pia elimu ya upandaji miti inatakiwa iendelee kutolewa katika ngazi zote nchini ili Watanzania wote wawe na uelewa wa upandaji miti na faida zake.

"Nashauri wataalamu wa Halmashauri zote nchini wakiona hili jambo linatekelezeka walifanyie kazi, tusiishie tu kutoa elimu kwa watu wachache, ikiwezekana tushuke mpaka ngazi za chini kabisa," alisema Boya.

Mwakilishi wa Shirika la Uhifadhi wa mazingira la WCS, Faraja Dembe ambao ndio walioandaa zoezi hilo, alisema shirika hilo limeandaa miti zaidi ya 100,000 kwa ajili ya kuipanda kwenye maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji.



Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi CCM Mbeya mjini, Afrey Nsomba akipanda mti kwenye chanzo cha maji za Nzovwe, zoezi ambalo linaratibiwa na Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi CCM kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya katika maadhimisho ya miaka 44 tangu kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi CCM. **PICHA GRACE MWAKALINGA.**

Alisema watahakikisha wanashirikiana na wadau wengine kupanda miti kwenye vyanzo vyote vya maji vilivyopo wilayani Rungwe na katika maeneo mengine ya Nyanda za Juu Kusini yenye uhitaji.

"Leo tunazindua hapa lakini tutaendelea kupanda miti hii kwenye vyanzo vingine vya maji, tumeandaa miti tofauti ya matunda na ya asili ambayo yote itapandwa kwenye maeneo tutakayoainisha," alisema Dembe.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema ili kuhakikisha upandaji miti unakuwa endelevu, wadau wanatakiwa kuwafundisha wananchi namna ya kuandaa vitalu vya miti kwenye maeneo yao badala ya kusubiri waandaliwe.

Alisema shughuli huyo itawasaidia kujipatia kipato kwa kuuza miche wanayoandaa na kushiriki kikamilifu utunzaji wa mazingira kwenye maeneo yao.

"Ukiona mtu kila siku anakuletea samaki ujuwe hakupendi, inatakiwa badala ya kukuletea samaki akufundishe kuvua samaki, sasa ninyi mnaoandaa hii miti wafundisheni wananchi namna ya kuiandaa, mtawasaidia kujipatia kipato na kushiriki kwenye utunzaji wa mazingira," alisema Chulya.

Baadhi ya wananchi walioshiriki zoezi hilo la kupanda miti katika chanzo cha maji cha Msasani, walisema miti hiyo ina faida kubwa kwenye maisha yao na hivyo wakaahidi kuitunza ili iwanufaishe katika miaka ijayo.

Mmoja wa wananchi hao, Ikupa Mwakanosya, alisema miti hiyo itawasaidia kutunza chanzo hicho cha maji na kuwafanya wapate maji mengi kwa muda mrefu.

Alisema watahakikisha wanailinda miti hiyo ili isiharibiwe ikiwamo kuzuia mifugo kuingia kwenye eneo hilo pamoja na kuzuia moto wakati wa kiangazi.

# TAMISEMI yaombwa kikao cha ujirani mwema na hifadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

LICHA ya operesheni ya kuondoa mifugo katika Bonde la Ihefu lililoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali kufanikiwa kwa asilimia 100, bado kuna hofu ya wafugaji hao kuirejesha mifugo hiyo hasa nyakati za usiku.

Hofu hiyo inakuja kutokana na idadi kubwa ya mifugo hiyo iliyoondolewa kwenye bonde hilo, lenye ardhi oevu kuhifadhiwa kwenye eneo huru (Buffer zone) ya hifadhi huku kukiwa hakuna maeneo ya kutosha kuchungia.

Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Mkoa wa Mbeya, imeiomba Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kusaidia kukabiliana na tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye ndiye aliyeanzisha oparesheni ya kuiondoa mifugo hiyo alisema idadi kubwa ya mifugo hiyo ilitoka katika mikoa ya Tabora, Singida na Shinyanga.

Alisema ili kukomesha tatizo hilo inatakiwa kuitishwa kikao cha ujirani mwema ambacho kitahusisha mikoa yote inayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo ni Mbeya, Iringa na Dodoma pamoja na mikoa mingine ya wafugaji.

"Tunamuomba Waziri wa TAMISEMI atusaidie kukaa na baadhi ya mawaziri wenzake ili watusaidie kutoa elimu itakayosaidia kukomesha tatizo hili la uingizaji wa mifugo kwenye hifadhi," alisema Chalamila.

Alisema kikao hicho kinatakiwa kuwashirikisha pia wafugaji ili kuhakikisha kunakuwepo na ulinzi shirikishi wa hifadhi hiyo ili kuokoa ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu ambayo imekuwa ikiharibiwa mara kwa mara.

Chalamila alisema ili kuhakikisha mifugo hiyo hairudi tena hifadhini, Serikali ya Mkoa kwa kushirikiana na maofisa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi nchini (TANAPA), wamewapeleka baadhi ya maaskari kwenye maeneo ya kuingilia mifugo ili kuhakikisha haiingizwi tena.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Izumbe Msindai, alisema kuondolewa kwa mifugo hiyo ndani ya hifadhi hiyo kutaleta manufaa kwa taifa kutokana na eneo hilo kuwa na umuhimu hasa kwa kutunza vyanzo vya maji vya mto Ruaha.

Alisema bonde hilo ni muhimu kwa kutunza maji yanayotumika kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo miradi ya kuzalisha umeme kwenye mabwawa ya Mtera, Kidatu na Nyerere.

Alisema miradi hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa hivyo kuondolewa kwa mifugo ndani ya bonde hilo kutasaidia kutekelezwa kwa manufaa miradi hiyo.

"Tulibaini kwamba idadi kubwa ya mifugo iliyoingizwa kwenye bonde hili siyo ya wafugaji wa Mkoa wa Mbeya baada ya kuwakamata baadhi yao na tulipowahoji tukabaini wanatoka mikoa mingine," alisema Msindai.

Aliishukuru Serikali ya Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano iliouonyesha kwenye zoezi hilo huku akiwaomba wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hiyo kuwa mabalozi wazuri.

# Barabara yafungwa kwa muda kisa hofu ya lori kuwaka moto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARABARA kuu ya Tanzania na Malawi, ililazimika kufungwa kwa zaidi ya saa moja juzi baada ya lori lililokuwa limebeba shehena ya mbolea kutoka jijini Dar es Salaam kwenda Malawi kuwaka moto kwenye mteremko wa Ilima wilayani Rungwe.

Lori hilo lilinusurika baada ya wakazi wa Kijiji cha Lubanda kushirikiana na dereva wa gari hilo pamoja na wapita njia wengine kuuzima moto huo kwa kutumia udongo na maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lubanda, Wema Mwakibibi, alisema wananchi walikuwa wapo majumbani mwao wakiendelea na shughuli zao na waliposikia mlio wa tairi kupasuka waliamua kukimbilia eneo la tukio ili kushuhudia kilichokuwa kimetokea.

Alisema wakati wanafika katika eneo hilo walikuta moshi umetanda kwenye lori hilo huku miale ya moto ikionekana na ndipo wakaanza kupambana na moto huo ili kuokoa gari hilo pamoja na mali zingine zilizokuwamo.

"Tulipofika hapa hatujataka kumjua dereva, utingo wake wala aina ya mzigo waliobeba, tumeona tuokowe kwanza mali na baada ya hapo tutarudi kumuuliza dereva," alisema Mwakibibi.

Alisema eneo hilo lina milima na miteremko mikali inayosababisha ajali kutokea mara kwa mara kwenye eneo hilo hasa magurudumu kupasuka hali ambayo inawafanya wananchi kuwa makini kufuatilia kila wanaposikia kishindo chochote.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lubanda, Usobi Sunday, alisema baada ya kusikia kishindo hicho waliamua kuwaondoa wanafunzi shuleni hapo na kuwapeleka mbali na eneo la tukio ili kuwaokoa.

Alisema waliamua kufanya hivyo baada ya kuona baadhi ya wanafunzi wakikimbilia eneo la ajali hiyo hali ambayo iliwatia hofu kutokana na matukio ya aina hiyo kuwahi kutokea na kuleta madhara kwa binadamu likiwamo la ajali ya Moto katika eneo la Msamvu mkoani Morogoro.

"Baada ya kuwaondoa wanafunzi tuliamua kusogea ili kuona nini kimetokea na ndipo tukakuta ni lori linawaka moto na tukaamua kushirikiana na wananchi kuchimba udongo wa kuzimia na kumwagilia maji mpaka tukafanikiwa kuzima," alisema Mwalimu Sunday.



# Mwinyi ataka CCM yenye uchumi imara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wakati umefika kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujipanga kiuchumi ili kiwe madhubuti kifedha.

Dk. Mwinyi ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, aliyasema hayo jana Mkoa wa Kusini Unguja alipokutana na viongozi wa chama hicho wa Mkoa huo.

Alisema Serikali iko katika mikakati ya kuhakikisha uchumi wake unaimarika na unakuwa mkubwa zaidi, hivyo chama nacho kinatakiwa kwenda sambamba na hali hiyo.

Alishauri kuanzishwa mfuko wa chama ili fedha zake zikisaidie na wanachama wake ambapo kwa kuanzia, amechangia Sh. milioni 20.

Alisema miongoni mwa majukumu aliyonayo ni pamoja na kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kusema kuwa atahakikisha ahadi zilizopo katika Ilaini hiyo anazitekeleza kwa vitendo.

Rais Dk. Mwinyi, alisema atahakikisha huduma bora kwa wananchi zinaimarika pamoja na kuzitekeleza ahadi alizozitoa kwa wajasiriamali wakati wa kampeni zake.

Pia alisema ahadi za wakulima wa mwani ambao aliwaahidi kuwatafutia masoko atahakikisha analifanyia kazi, kilimo cha mpunga, matatizo ya mradi wa mpunga Cheju nayo itafanyiwa kazi ili wakulima wa bonde hilo walime vizuri.

Kwa upande wa wavuvi, alisema atahakikisha sekta hiyo inaimarika hasa ikizingatiwa kipaumbele zaidi cha uchumi wa serikali hivi sasa umejikita katika uchumi wa buluu, hivyo wavuvi watapata fursa ikiwamo ujenzi wa bandari ya uvuvi ambayo itajumuisha viwanda vya kusindika samaki, chuo cha kufundisha mabaharia ambavyo vitajengwa katika eneo hilo.

Kuhusu ajira, alisema katika Ilani ya CCM imeelezwa kuna ajira 300,000 zitakazotolewa, kazi ambayo inatekelezwa ikiwamo kuhakikisha inaanzishwa miradi mikubwa ambayo itazaa ajira, ukiwamo mradi wa bandari na viwanda.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdalla Juma Mabodi, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa hatua anazozichukua ikiwamo kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Wenyeviti wa Mkoa huo waliipongeza ziara ya Rais Dk. Mwinyi katika Mkoa huo pamoja na kumpongeza kwa uteuzi wake wa viongozi.

Aidha, viongozi hao waliahidi kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupongeza juhudi anazozichukua katika kuiongoza Serikali kwa uzalendo, ari na kupambana na ufisadi, wizi na rushwa.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, akizindua rasmi Chama cha Madaktari Bingwa wa Maradhi ya Saratani Tanzania mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR.**

# SMZ yakoshwa na wataalamu wa afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdalla, amesema Serikali ya Zanzibar na Tanzaina zinathamini mchango mkubwa unaotolewa na wataalamu wa afya na zitaendelea kuboresha mazingira yao.

Lengo ni kuwawezesha kutoa huduma bora zaidi na kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi mbalimbali.

Aliyaeleza hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Chama cha Madaktari Bingwa wa magonjwa ya saratani Tanzania uliofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema kuanzishwa kwa chama hicho ni kitu cha kujivunia na inaelekea lengo ni kwenda mbali zaidi katika mapambano dhidi ya maradhi hayo ambayo yamekuwa yakiongeza kwa kasi.

Aliwahakikishia wanachama wa Chama hicho kwamba Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitaendelea kushirikiana na Chama hicho kuhakikisha huduma za matibabu ya maradhi ya saratani zinaimarishwa.

Hemed alisema virusi vya maradhi ya saratani kama vilivyo vya maradhi mengine vimekuwa vikibadilika, hivyo kuwapo kwa taasisi, wanachama wake watafaidika na ujuzi unaoendana na mabadiliko yanayotokea katika tiba ni jambo zuri.

Aliwashauri madaktari bingwa wa maradhi ya saratani ambao hawajajiunga na chama hicho wajiunge kutokana na faida nyingi zinazopatikana kutoka taasisi nyingine za kitaaluma.

Alieleza saratani ni moja ya magonjwa hatari yasiyoambukiza na inakadiriwa watu takribani milioni 7.9 hufariki kila mwaka duniani ikiwa ni sawa na asilimia 21 ya vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza, na kwamba zaidi ya theluthi mbili ya wagonjwa hao wanagunduliwa katika nchi zinazoendelea.

Makamu wa Pili wa Rais alibainisha kwa Tanzania saratani inashika nafasi ya tano kwa wanaume na ya pili kwa wanawake kusababisha maradhi na vifo.

Aliitaja saratani ya shingo ya kizazi kuwa inaongoza ikifuatiwa na ya matiti na ngozi kwa wanawake na upande wa wanaume ni ya ngozi, kichwa na tezi dume.

Naye Rais wa Chama hicho, Dk. Jerry Ndumbalo, alisema lengo la chama chao ni kuisaidia Serikali katika kuimarisha matibabu na kufanya kampeni ya kuchunguza saratani katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ili kuigundua katika hatua za awali na kuwapatia matibabu.

## Kibano kwa wauza vileo chatangazwa

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya ushauri na udhibiti wa vileo Zanzibar, imewataka wamiliki wa baa,wauzaji wa vileo na wenye hoteli za kitalii kukata leseni ili kuwa na uhalali wa kufanya biashara hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Abdulrazak Abadulkadir Ali, alisema bodi hiyo imepokea maombi ya wafanyabiashara wa vileo 218 na waliokata leseni na kupewa vibali vya kuendesha shughuli hiyo hadi kufikia mwishoni mwa Januari mwaka huu ni 126.

Alisema bodi hiyo imeazishwa chini ya kifungu cha nane cha sheria namba tisa cha mwaka 2020 na ina jukumu la kuhakikisha inadhibiti uuzaji, uagizaji, uhifadhi, utumiaji na usambazaji wa vileo pamoja na kusimamia maombi, utoaji, ulipaji upya wa leseni na vibali vya uagizaji vileo na kuwachukulia hatua wanaoendesha biashara hiyo bila kufuata sheria.

Mwenyekiti huyo alisema ni jukumu la wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa Serikali za mitaa, vyombo vya ulinzi na usalama na wananchi kwa ujumla kushakikisha wanashirikiana na bodi hiyo kuwafichua wanaoendesha biashara ya vileo kinyume cha utaratibu ili hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

“Bodi inasisitiza kuwa wadau wote wafuate sheria bila ya kushurutishwa na kuepuka usumbufu na pia kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi,” alisema Mwenyekiti huyo.

Aidha, alisikitishwa kuona baa ambazo zinamilikiwa na vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo Polisi Mesi na ya Nyuki ambayo inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ, hazijakata leseni na zinaendelea kufanya biashara, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

# Wenye ulemavu wasiochukua mikopo halmashauri kusakwa

**Na Happy Severine,** SIMIYU

SERIKALI imewataka wa wenye ulemavu kujitokeza kuchukua mikopo inayotolewa na halmashauri bila riba ili kuondokana na adha ya kutumikishwa na watu wengine kama ombaomba ndani na nje ya nchi.

Wito huo umetolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, alipokutana na kuzungumza na makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu katika Mkoa wa Simiyu.

Lengo la kukutana na makundi hayo ni kujadili mbinu za kukabiliana na changamoto zinazowakabili badala ya kujiingiza katika makundi mabaya mtaani likiwamo la ombaomba.

Nderiananga alisema licha ya halmashauri kutenga asilimia mbili ya mapato kwa ajili ya watu wenye ulemavu, makundi hayo yameshindwa kujitokeza kuchngamkia fursa hiyo.

"Nitoe wito kwa watu wenye ulemavu kujitokeze kwenda halmashauri kuchukua fedha ambazo mmetengewa na serikali ili kuepukana na adha ya kutumikishwa kama ombaomba wa ndani na nje ya nchi," alisema Nderiananga na kuongeza:

"Imebainika kuwa licha ya serikali kutenga fedha hizo kwa watu wenye walemavu, hawajitokezi kuchukua na ili kuepukana na tatizo hilo, nitaanza msako wa kuwasaka wote wasiotoka kwenda kuchukua fedha zao, kwani tunawategemea katika kuongeza pato la taifa."

Aidha, aliwataka waliochukua mikopo hiyo kuitumia kuzalisha na kurejesha kwa mujibu wa utaratibu ili watu wengine wapewe.

Katibu wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Simiyu, Alex Benson, aliomba walemavu kutengewa posho ili kuwanusuru na vitendo vya kuomba omba mtaani.

Mwenyekiti wa Watu wenye Ulemavu wa Viungo CHAWATA), Mkoa wa Simiyu, Gera Makasi, alieleza kuwa kundi hilo hawana elimu juu ya fedha zinatolewa kwa ajili yao, hivyo kushindwa kujitokeza kuchukua mikopo hiyo.



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori, akizungumza wakati akifunga mafunzo kwa makandarasi wazalendo kuhusu namna ya kuomba zabuni kupitia mtandao na namna ya kusoma mikataba vizuri, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ummy awaonya wataalamu elekezi wasio waaminifu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu ametoa onyo kwa wataalamu elekezi wasio waaminifu kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwani wamekuwa wakirudisha nyuma juhudi za serikali za kuvutia uwekezaji nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa ameambatana na Waziri mwenzake wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa (NEMC), Dk Samuel Gwamaka, baada ya kutembelea na kukagua mazingira ya kiwanda cha BTY kinachochakata taka hatarishi zinazotokana na betri kilichopo Buguruni jijini Dar es Salaam ambapo uzalishaji wake ulisimamishwa kutokana na kutokidhi taratibu za mazingira, Waziri Ummy alisema mwekezaji huyu amekwamishwa na mtaalamu elekezi kwa kushindwa kuwasilisha tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) kabla ya mradi kuanza.

"Nitafuta vibali vya wataalamu elekezi wote wasio fuata taratibu za kazi zao ikiwa ni pamoja na kutokuwa waaminifu kwani kufanya hivyo kunarudisha nyuma juhudi za Serikali katika kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025," alisema Waziri Mwalimu.

Alisema Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji kwa wazawa na wageni kutoka nje ya nchi, hivyo ni muhimu kuhakikisha jitihada hizi hazikwamishwi ili kufikia malengo ya Serikali.

"Tunahitaji wataalamu elekezi wenye sifa zinazosaidia kuitangaza nchi vizuri jambo ambalo litachochea uwekezaji hapa nchini. Wizara pamoja na NEMC. hatutakubali kufanya kazi na wataalamu elekezi ambao watakiuka matakwa ya ufanyaji wa kazi zao," alieleza.

Katika Hatua nyingine, Waziri Mwalimu aliwata NEMC kukutana na Uongozi wa Kiwanda cha BTY na kuwapa mwongozo utakaokifanya kiwanda kuendelea na uzalishaji sambamba na utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Waziri alizitaka taasisi zote zinazohusika moja kwa moja na uwekezaji kuacha tabia ya kufanya kazi za polisi na badala yake zifanye kazi kama washauri hali ambayo itaongeza kasi ya uwekezaji.

"Nitumie nafasi hii kuziasa taasisi zote zinazohusika na uwekezaji kufanya kazi za kiushuri zaidi badala ya kufungia viwanda vinapoonekana vimekiuka kanuni, sheria na taratibu za nchi kwani kufanya hivyo kunapoteza mapato yanayotokana na kodi pamoja na ajira kwa vijana wetu," alisema.

Kwa upande wake Waziri wa Viwanda na Biashara, . Mwambe alisema uwapo wa shughuli nyingi za kunaongeza wigo wa walipa kodi hali ambayo huimarisha uchumi wa nchi.

"Viwanda vinapokuwa vingi ndani ya nchi vinaongeza wigo wa walipa kodi ambapo kodi hizo husaidia kujenga miradi mbalimbali ikiwemo miundombinu na uboreshaji wa huduma mbalimbali. Tunaamini changamoto tulizozikuta hapa zitapatiwa ufumbuzi na pande zote kunufaika," alisema Mwambe.

Naye Gwamaka aliwashauri wawekezaji kutafuta wataalamu elekezi wenye weledi na waadilifu na hata wanapokutana na changamoto ya kuwapata basi wafike ofisi za NEMC makao makuu au ofisi za kanda kwa ushauri zaidi.

"Mawaziri wametutaka uongozi wa NEMC ndani ya siku mbili kukutana na mwekezaji kwa ajiri ya kutoa maoni yetu ya kitaalamu na tutafanya hivyo kupitia timu ya wataalamu iliyopo.

## Mikakati ya kufufua pamba yashika kasi

**Na Idda Mushi,** ULANGA

MIKAKATI ya kuhakikisha kilimo cha pamba kinafufuliwa mkoani Morogoro na Kanda ya Mashariki imeendelea kushika kasi, baada ya wadau wa maendeleo zikiwamo taasisi za kifedha kuanza kuonyesha nia kusaidia kilimo hicho.

Hatua hiyo imetokana na kilimo hicho kuwa na faida kubwa kiuchumi kwa taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Miongoni mwa taasisi za kifedha zilizoonyesha nia ya kusaidia kilimo hicho ni Benki ya CRDB waliotembelea eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kipya cha kuchambua pamba kilichopo eneo la Lupiro wilayani Ulanga mkoani Morogoro.

Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuona uwezekano wa kushirikiana na wawekezaji ili zao hilo liweze kumnufaisha mwananchi kiuchumi na Taifa kwa ujumla.

Meneja wa Benji ya CRDB Wilaya ya Ulanga, Godwin Lukumai, alimwakilisha Mkurugenzi wa CRDB Mkoa wa Morogoro kukagua eneo hilo na kubainisha kama taasisi ya kifedha wameamua kutembelea eneo hilo kujionea hali halisi na kupata maelezo ili kuangalia watakavyoweza kushirikiana na mwekezaji kuinua upya kilimo cha zao hilo mkoani Morogoro.

Kwa Upande wake Mkaguzi wa pamba kwa wilaya za Ulanga na Malinyi, Alfred Chagula, alisema Kampuni ya Upami Agro Business ambayo ndio wanunuzi wa zao hilo Kanda ya Mashariki imelenga kushirikiana na Serikali na wananchi kufufua zao hilo kwa kuondoa changamoto mbalimbali zilizofifisha kilimo hicho mkoani Morogoro ikiwamo kero kubwa ya muda mrefu ya ukosefu wa masoko ya uhakika kwa Kanda ya Mashariki.

## HABARI KIMATAIFA

### Waipinga sheria usalama wa taifa

**Paris,** UFARANSA

MAELFU ya waandamanaji wamejitokeza katika miji kadhaa nchini hapa, kupinga muswada wa usalama ambao utawazuia watu kurekodi na kuchapisha video zinazohusiana na ukatili wa polisi.

Kulingana na waandaaji wa maandamano hayo, kulikuwa na mikusanyiko zaidi ya 55 wakiandamana.

Wanaharakati wa vuguvugu la Fulana za Manjano lililoshika kasi kwa zaidi ya mwaka mmoja Ufaransa, walishiriki kwenye maandamano hayo. **DW**

### Ndege ya rais yatua kwa dharura

**Washington,** MAREKANI

NDEGE iliyombeba Rais wa Ecuador, Lenin Moreno ilitua kwa dharura mji mkuu wa Washington, Marekani.

Sababu ya kutua ndege hiyo ni matatizo katika mitambo. Ilielezwa kuwa kiongozi wa Ecuador, alifanya ziara rasmi nchini Marekani na kwamba tukio hilo lilitokea baada ya ziara hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa, Moreno na wafuasi wake wana hali nzuri. Hakuna taarifa iliyotolewa kuhusu chanzo cha kushindwa kwa mitambo. **TRT**

### Polisi wauawa wakishambuliwa

**Nangarhar,** AFGHANISTAN

POLISI wanane, wameuawa katika shambulizi la bomu katika Mkoa wa Nangarhar, mashariki mwa Afghanistan.

Pia katika tukio lingine, raia wanne walijeruhiwa katika shambulizi jingine Kabul.

Msemaji wa Gavana wa Nangarhar, Ataullah Hogyani, aliwaambia waandishi wa habari kwamba washambuliaji walilenga kituo cha polisi katika wilaya ya Gandumak wilayani Shirzad na gari lililokuwa limetegwa bomu.

Hogyani alisema kuwa maofisa wanane wa polisi walipoteza maisha katika shambulizi hilo. Ubaidullah Shinvari, Naibu Mkuu wa Mkoa wa Nangarhar Shura, alidai kuwa maofisa 14 wa polisi walifariki. **TRT**

# Maelfu wafuasi wa Navalny mikononi mwa Polisi

**Moscow,** URUSI

WAANDAMANAJI takribani 1,000, waliojitokeza barabarani, kudai kuachiliwa kwa kiongozi wa upinzani aliyefungwa jela, Alexei Navalny, wamekamatwa.

Wimbi la maandamano ya kitaifa yametikisa maeneo kadhaa, Ikulu ya Kremlin. Mamlaka nchini Urusi, zilifunga vituo vya treni na basi vya abiria na kuzuia shughuli za watu katika mji mkuu wa nchi hiyo Moscow kabla ya mkutano maandamano makubwa yaliyopangwa kumuunga mkono kiongozi huyo.

Migahawa, maduka katikati ya mji huo yalifungwa, huku zaidi ya watu 4,000 tangu wiki iliyopita, walikamatwa nchini kote, wakati wa mikutano.

Navalny (44), alifungwa jela aliporejea nchini Urusi baada ya kupona jaribio la kuuawa kwa sumu inayoua neva.

Mpinzani huyo wa serikali ya Urusi, alitakamtwa Januari 17, mwaka huu kwa kutotimiza masharti ya hukumu iliyoahirishwa dhidi yake.

Alikuwa amewasili kutoka mjini Berlin, ambako aliishi kwa miezi kadhaa akiendelea kupona shambulio la sumu.

**Maandamano makubwa ya kumuunga mkono Navalny, yalianza kufanyika Urusi, licha ya onyo jipya kutolewa na polisi kuhusu mikusanyiko ya watu.**

Mamlaka nchini Urusi, zilisema kuwa alipaswa kuripoti polisi kwa sababu ya kesi yake ya ubadhilifu wa mali ya umma, iliyoahirishwa.

Navalny alipinga kukamatwa kwake akisema ni ukiukaji wa sheria na kuongeza kuwa mamlaka zinafahamu kwamba alikuwa akitibiwa mjini Berlin kutokana na sumu ya Novichok, ambayo alipewa Urusi, Agosti mwaka jana.

Maandamano makubwa ya kumuunga mkono Navalny, yalianza kufanyika Urusi, licha ya onyo jipya kutolewa na polisi kuhusu mikusanyiko ya watu.

Kwa mujibu wa kikundi cha maandalizi ya maandamano hayo OVD-Info protest monitoring group, maandamano katika mji mkuu Moscow yanatarajiwa kufanyika tena.

Washirika kadhaa wa Navalny wamekuwa wakifungwa tangu juma lililopita akiwamo kaka yake na mwanaharakati wa kikundi cha Pussy Riot Maria Alyokhina, ameweka katika kifungo cha ndani.

Mhariri Mkuu wa Wavuti wa Urusi uliobobea katika masuala ya Haki za Binadamu, Sergei Smirnov, alikamatwa nje ya nyumba yake, Jumamosi.

Taarifa za kukamatwa kwake kutokana na tuhuma za kushiriki katika maandamano ya wiki iliyopita, zimelaaniwa vikali na waandishi wa habari, nchini humo.

Vituo saba vya safari za leri vilifungwa jana na matembezi ya raia yalidhibitiwa katikati mwa mji wa Moscow, limeripoti Shirika la Habari la AFP.

Maandamano yanatarajiwa katika maeneo mengine ya nchi, licha ya kuwapo baridi kali baada ya viwango vya joto kushuka hadi nyuzijoto -52.

Utawala wa Kremlin ulikanusha kuhusika shambulio la sumu kwa mpinzania huyo na kupinga matokeo ya uchunguzi ya wataalamu wa silaha kutoka nchi za Magharibi, kwamba sumu aina ya Novichok ilitumika dhidi ya Navanly. **REUTERS/BBC**



Maofisa wa polisi wakiwa wamemkamata mwandamanaji wakati wa maandamano dhidi ya kifungo cha kiongozi wa upinzani, Alexei Navalny, Moscow, Urusi, jana. Maelfu waliandamana wakidai kuachiliwa kwa kiongozi huyo. **PICHA:**

# Timu ya WHO yatua eneo chimbuko la corona China

**Wuhan,** CHINA

TIMU ya wataalam kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), imetembelea la soko la Huanan lililopo katikati ya jiji la Wuhan, kulikogundulika kirusi cha kwanza cha corona.

Soko hilo lilikuwa la jumla ya bidhaa za baharini ikiwamo samaki, lilifungwa baada ya kugundulika ugonjwa wa Covid-19 unaotokana na virusi hivyo. Timu hiyo iliwasili katika soko hilo huku kukiwa na ulinzi mkali na kuwekwa vizuizi, ilitumia saa moja kisha kuondoka mjini Wuhan, ulio na takribani wakazi milioni 11.

Timu hiyo, tangu kutolewa kutoka karantini ya wiki mbili, imetembelea hospitali, masoko pia maonyesho ya kuwakumbuka waliokumbwa na corona pamoja watu kuzuiwa kwa siku 76.

"Ziara ilikuwa muhimu sana leo katika soko la jumla la Huanan. Muhimu kwetu kuelewa ugonjwa Covid-19 ulianza hapa na kuenea mwishoni mwa mwaka 2019, "mmoja wa wataalamu hao, Peter Daszak aliandika kwenye Twitter.

Desemba 31, mwaka 2019, baada ya visa vinne vya homa ya mapafu kutokea sokoni hapo, lilifungwa mara moja, hadi Januari, mwaka huu, Wuhan ilikuwa imeingia katika siku 76 za kufungiwa.

Wataala walisema soko la Huanan bado lina jukumu la kutafuta asili ya virusi hivyo. **REUTERS**

# MAN CITY YAWEKA REKODI MPYA EPL



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City imeweka rekodi mpya ya kushinda mechi 12 mfululizo kwenye mashindano yote baada ya kuifunga Sheffield United bao1-0 juzi, Jumamosi.

Bao hilo la mapema kutoka kwa Gabriel Jesus na kufikisha mechi 12 za Ligi Kuu bila nyavu zake kutikiswa kulikisaidia kikosi hicho cha Pep Guardiola kupata ushindi ulioifanya kuongoza ligi kwa tofauti ya pointi nne.

Ushindi huo mfululizo ni mrefu zaidi tangu Arsenal ilipofanya hivyo kati ya mwaka 2007.

Pia kumeipa nafasi nzuri timu hiyo, ambayo sasa imeanza kuona majeruhi wake wakirudi dimbani.

Ikiwa pia ipo kwenye fainali ya Kombe la EFL na kweye hatua ya tano ya Kombe la FA.

Kiukweli sasa, City mafanikio hayo ni makubwa zaidi kwake tangu kuundwa kwa ligi hiyo mwaka 1888.

# Rashaford akumbana na ubaguzi England

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford, mshambuliaji wa Klabu ya Manchester United amesema anatambua kwamba ana rangi nyeusi na anaifurahia, hivyo wale wanaombagua hawatendi jambo la haki na wala wasifikiri kwamba atawajibu.

Nyota huyo wa Manchester United alikutana na jambo hilo kupitia mitandao ya kijamii muda mfupi baada ya timu yake kulazimisha sare ya bila kufungana dhidi ya Klabu ya Arsenal, Uwanja wa Emirates kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Kupitia kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram mashabiki walianza kumshambulia Rashford kwa kutumia 'emoji' za nyani na wengine waliweka ujumbe kwamba anapaswa kwenda maeneo ya makazi ya wanyama jambo ambalo limemuumiza nyota huyo kuhusu ubaguzi wa rangi.

Mbali na Rashford mwenye miaka 23, pia suala hilo la ubaguzi wa rangi lilimtokea nyota mwenzake Axel Tuanzebe na Anthony Martial pia nyota wa Chelsea Reece James na nyota wa Klabu ya West Broms Romaine Sawyer nao pia walikutana na ubaguzi kwenye mitandao ya kijamii.

Rashford kupitia tweet amesema: "Utu na mitandao ya kijamii umekuwa kwenye wakati mbaya kwa sasa. Ndio ninajua kwamba mimi ni mweusi na ninaishi katika hilo ninajivunia kabisa kwa rangi ambayo ninayo.

"Hapana, hapana, ujumbe wowote ambao utauandika hapa ama hakuna mtu yeyote yule ambaye anaweza kunifanya nijiskie tofauti.

"Samahani ikiwa unahitaji kuona ninaweza kuchukulia tofauti hilo haliwezi kutokea kwangu kwa wepesi tu, hautaona kwangu samahani. Kuna watoto wazuri ambao wanaipenda rangi yangu na wanafuata ndoto zao siwezi kuwaangusha."





# Klopp akubali beki anahitajika Liver

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekubali Liverpool inahitaji kuleta nyongeza ya mchezaji kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa leo lakini ikiwa tu wachezaji sahihi wakipatikana.

Pamoja na Virgil van Dijk kutopatikana katika timu ya Liverpool, Klopp amekuwa akimtumia Fabinho kama beki wa kati wa muda.

Lakini Mbrazil huyo hakucheza katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Tottenham kutokana na jeraha kidogo la misuli na Joel Matip alilazimishwa kutoka wakati wa mapumziko baada ya kupata maumivu ya mishipa ya kifundo cha mguu.

Na wakati Jordan Henderson amepelekwa kama mlinzi wa dharura, mabingwa watetezi hao wanakosa uzoefu sana upande wa nyuma.

Klopp alisema: "Unaweza kufikiria kwamba tunafikiria juu ya kila kitu mambo magumu.

"Kwa kweli, tulifikiri wakati wote, tunafikiria wakati wote, ni juu ya kufanya jambo sahihi.

"Kiukweli kwa sasa tunahitaji kupata mchezaji anayefaa.

"Tuna wachezaji, bado sio wengi kuwa na uzoefu katika safu ya ulinzi, ni jambo la kushangaza ni nini kinatokea huko. Ni jambo la kushangaza sana."

HABARI MICHEZO

# Dembele mbadala wa Sancho United

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wanaripotiwa kuwa wanajaribu kumsajili, Ousmane Dembele kutoka Barcelona ikiwa watashindwa tena kukamilisha uhamisho wa Jadon Sancho wa Borussia Dortmund.

'Mashetani Wekundu' hao walihusishwa sana na Sancho wakati wa msimu uliopita wa majira ya joto, lakini hawakuweza kufikia makubaliano na BVB, ambao wanaaminika walikataa kushusha bei yao ya pauni milioni 108.

Kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer pia kilisemekana kipo mbioni kufanya makubaliano ya mkopo kwa Dembele, lakini dirisha la uhamisho lilifungwa na mchezaji huyo wa Ufaransa bado akiwa Camp Nou.

Inatarajiwa Dembele bado ataendelea kuwa vichwani mwa United, kama mbadala wa Sancho ikiwa dili hilo litaendelea kwenda mrama.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Bild, Christian Falk, mabingwa hao mara 20 wa Uingereza bado wanavutiwa na mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa na wanaweza kufanya biashara ikiwa watashindwa kufikia makubaliano juu ya Sancho.

Dembele amekuwa kwenye kiwango cha kawaida kwenye kikosi cha Ronald Koeman katika msimu wa sasa, akiwa amecheza mechi 21 kwenye mashindano yote, akichangia mabao sita na pasi tatu za mwisho mzimu huu.

Sancho, wakati huo huo, amecheka na nyavu mara mbili tu kwenye Bundesliga msimu huu, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa England ana rekodi ya mabao sita na pasi za mwisho 13 katika safari za mechi 23 kwa jumla.





# MOURINHO: NI MUDA KWA BALE KUONYESHA MAKALI

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema wakati umefika kwa Gareth Bale kujitokeza na kuonyesha anastahili nafasi yake katika kikosi cha Tottenham.

Kufungwa kwa Spurs na Liverpool Alhamisi iliyopita kulichangiwa na habari kwamba mshambuliaji nyota, Harry Kane anakabiliwa na jeraha la kifundo cha mguu na atakaa nje ya dimba kwa wiki kadhaa.

Kikosi cha Mourinho kilikosa mashuti yoyote ya ushambuliaji na Kane hakuhusika katika kipindi cha pili kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur, na matumaini yao ya ubingwa yanaweza kufifia kama hatokuwapo.

Kocha anahitaji majina yake makubwa yaliyobaki ili kufanya uwapo wao katika mbio za kuwania ubingwa.

Son Heung-min ametoa kiwango thabiti na huenda akaendelea na moto huo huo, lakini alama za viulizo zinaendelea juu ya Bale kufuatia uhamisho wake wa mkopo kutoka Real Madrid msimu uliopita.

Alifika kwa mashabiki wengi, lakini awamu yake ya pili kwenye klabu bado hajaondoka. Kukosekana kwa Kane kunatoa nafasi ya kushambulia pembeni, na Mourinho amemtaka nahodha wa Wales kuichukua.

"Ni wakati muhimu kwake Gareth Bale, anajisikia vizuri na bora," alisema Mourinho.

# *Liverpool wamalizana na Aaron Long*

**LIVERPOOL,** England

IMERIPOTIWA kuwa Klabu ya Liverpool ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, wamemalizana na beki wa kati wa Klabu ya New York Red Bulls, Aaron Long.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Liverpool kutokuwa imara upande wa ulinzi kutokana na mabeki wake wengi kuwa majeruhi ikiwa ni pamoja na Virgil van Dijk ambaye ni beki kisiki wa kati na Joe Gomez wanaotarajiwa kukaa nje msimu mzima wakitibu majeraha yao.

Pia Joel Matip aliumia kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Tottenham, hivyo naye anasumbuliwa na majeraha jambo ambalo linawafanya Liverpool wasiwe na chaguo zaidi ya kuhitaji saini ya beki huyo mwenye miaka 28 kwa mkopo.

Jurgen Klopp, Kocha Mkuu wa Liverpool amesema kuwa watafanya jitihada ili kuweza kuwa imara katika safu ya ushambuliaji pamoja na ulinzi ambavyo vyote vinategemeana ndani ya uwanja.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AFURAHIA SARE ARSENAL MBIO UBINGWA

●●● Unaangalia kila mchezo, tuliyocheza dhidi ya Arsenal, Chelsea, City, Liverpool, tulijilinda vema...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United wamepata imani kubwa zaidi kwenye malengo yao ya kuwania taji la Ligi Kuu England baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Arsenal, Jumamosi.

**'Mashetani Wekundu' hao, siku tatu zilizopita walikumbana na kipigo nyumbani kutoka kwa Sheffield United, na kisha juzi wakashindwa kutumia nafasi yao kushinda dhidi ya 'Washikabunduki' hao dhaifu waliopo chini ya kocha, Mikel Arteta.**

Alexandre Lacazette aligongesha mwamba kwa mkwaju wa adhabu ndogo, lakini Edinson Cavani alikosa pengine nafasi mbili bora zaidi kwenye mchezo huo, wakati United wakicheza mchezo wa tano na timu kubwa sita bila kufunga bao.

Sare hiyo maana yake ni kwamba kikosi cha Solskjaer kwa sasa kimepitwa pointi tatu na Manchester City, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Ingawa Solskjaer hakutaka kuzungumzia nafasi yao ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2012-13, alisisitiza wachezaji wameuweka moyoni mchezo kutoka Uwanja wa Emirates.

"Hatuzungumzii kuhusu mbio za ubingwa au ubingwa wa sasa, tuko Januari," alisema. "Tunachokiwaza kwa sasa ni kujipanga ili kurudi kwenye njia yetu.

"Tulikatishwa tamaa Jumatano, leo tumepata imani tena kwa sababu tunahisi tulitawala mpira na tulikuwa na nafasi kubwa ya kushinda.

"Lakini huwezi kuyatawala matokeo na mtazamo wa mchezo wenyewe, ingawa ulikuwa mzuri sana.

"Bila shaka, unaangalia kila mchezo, unaangalia michezo tuliyocheza dhidi ya Arsenal, Chelsea, City, Liverpool, tulijilinda vema na kwa uhakika tulikuwa na nafasi ya kufunga.

"Hiyo ndio nguzo kubwa ya kucheza. Tunahitaji kuchukua nafasi yetu na tunajua kwamba, bado haijafanya vizuri sana kwa sasa."

## ZISIKUPITE

### RAMOS AITAMANI UNITED

MLINZI wa Hispania, Sergio Ramos, 34, yupo tayari kuondoka Real Madrid na anataka kwenda Manchester United. ***(Mirror)***

### ARSENAL KUMNUNUA AANHOLLT

ARSENAL inapanga kumsajili mlizi wa pembeni wa Crystal Palace, Patrick van Aanholt, 30, raia wa Uholanzi. ***(Mirror)***

### BROMS WAKOMAA NA BENTEKE

KLABU ya West Brom inataka kumsajili straika wa Crystal Palace, Christian Benkeke, 30, raia wa Ubelgiji. ***(Sun)***

### DEMBELE KUKOMAA BARCA

WINGA wa Barcelona, Ousmane Dembele, 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Chelsea na Juventus, anataka kubaki Nou Camp. ***(Sport)***

### AURIER NA MAJALIWA SPURS

MLINZI wa kulia wa Ivory Coast, Serge Aurier, 28, anapigania nafasi yake pale Tottenham baada ya kukosa nafasi kwenye kikosi hicho. ***(Mail)***

### ROJO KWENDA BOCA JUNIORS

MLINZI wa Argentina, Marcos Rojo, 30, anatarajia kuvunja mkataba wake na Manchester United ili atue kule kwa miamba ya Argentina, Boca Juniors akiwa mchezaji huru. ***(Sky Sports)***

### YEDLIN KUTUA GALATASARAY

MLINZI wa Newcastle United raia wa Marekani, DeAndre Yedlin, 27, anatarajia kutua Ligi Kuu Uturuki katika Klabu ya Galatasaray. ***(ESPN)***

### ROSE MAMBO MAGUMU

MLINZI wa kushoto wa Tottenham na England, Danny Rose, 30, uhamisho wake wa kwenda Trabzonspor unaweza kushindikana, baada ya klabu hiyo kusema haitaweza kumnunu. ***(Talksport)***

### UNITED WAMTAKA KOUNDE

MANCHESTER United inajaribu kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa Sevilla, Jules Kounde, 22, kwa pauni milioni 60. ***(Mirror)***

### DALOT KUNUNULIWA JUMLA

AC Milan inataka kumsajili mlinzi wa kulia wa Manchester United, Diogo Dalot, 21, kwa pauni milioni 15. Mchezaji huyo ambaye ameiwakilisha Ureno kwenye kikosi cha taifa chini ya umri wa miaka 21, ameonyesha kuwavutia. ***(Sun)***

### TOSUN KUTUA BESIKTAS

STRAIKA wa Everton, Cenk Tosun, 29, jana Jumapili alikuwa mjini Istanbul kukamilisha uhamisho wake wa kutua Besiktas. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

## Mtibwa kupigania 21 za nyumbani

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thierry Hitimana, amesema hapendi kuona timu yake ikicheza mechi ya mchujo ('Play off') kupambania kubaki Ligi Kuu Bara, hivyo anataka kuhakikisha wanafanya vizuri na kumaliza katika nafasi saba za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo mzunguko wa pili unatarajia kuanza wiki ijayo, Februari 13.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Hitimana alisema watapigania kupata pointi 21 katika mechi saba za nyumbani kwenye mzunguko wa pili ili kujiweka katika nafasi nzuri.

Alisema ana michezo 17 kati ya hiyo, saba watakuwa nyumbani, ambayo anafanya kazi kubwa na wa wachezaji kuhakikisha wanapambania kuvuna pointi zote 21 ambazo anaamini zitawaweka katika mazingira mazuri.

## Dube apunguziwa majukumu Azam

**Na Saada Akida**

HUKU akicheka na nyavu mara mbili wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya KMC FC iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wamempunguzia majukumu mshambuliaji wao, Price Dube ikiwamo kutopiga na kucheza katikati.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema baada ya Dube kutoka chumba cha majeruhi, nyota huyo ameanza kucheza na wakimpunguzia baadhi ya majukumu ili kumuepusha na uwekano wa kuumi tena.

Alisema sasa Dube atakuwa akipewa majukumu mengine ikiwamo kucheza pembeni ili kupunguza purukushani za kugongana na mabeki.




Washiriki wa mbio za NIC Goba Hills Marathon, wakijiandaa kuanza mbio hizo zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# MBIO ZA NIC GOBA MARATHON ZAFANA, MAELFU WASHIRIKI

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za NIC Goba Hills Marathon ambazo zimefanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, zimefana sana huku wadhamini wakuu ambao ni Kampuni ya Bima ya Tanzania (National Insurance Corporation) wakiahidi kuendelea kuzidhamini kwa miaka mingine mitatu ijayo.

**Huku zikiwa na kauli mbiu ya "Kimbia, Okoa Maisha ya Mama na Mtoto" na ikiwa ni msimu wake wa pili, mbio za NIC Marathon ambazo zilifanyika Shule ya Sekondari ya Goba mwaka huu zaidi ya watu 3,000 walijitokeza kushiriki.**

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema kampuni hiyo inajivua kuwa mdhamini mkuu wa mbio hizo na itaendelea kuzidhamini.

"Ni furaha sisi kuwa wadhamini wakuu wa mbio hizi kwani malengo yetu ya kuzidhamini yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana," alisema Doriye.

Doriye aliongeza kuwa lengo kubwa la kudhamini NIC Goba Hills Marathon ni pamoja na kuunga juhudi za serikali ya tano ya kutambua vipaji vya vijana pamoja na kuvikuza.

"Tunaelewa kwamba michezo ni ajira, tunao vijana wengi ambao wamejipatia kipato chao cha kila siku kutokana na michezo. Moja ya juhudi kubwa ambazo serikali ya awamu ya tano inafanya ni pamoja na kuunga juhudi za vijana kwenye kujiajiri na ndio sababu sisi NIC tumedhamini mbio hizi ili kutambua na kukuza vipaji vya vijana wetu waweze kujiajiri kwa kupitia michezo," alisema Doriye.

Mbio hizo zilikuwa za Kilomita 42.2 (Full Marathon), Kilomita 21.1 (Half Marathon), Kilomita 10 (Corporate Run) na Kilomita tano (Family Run) kwa wanaume na wanawake. Mshindi wa Kilomita 42.2 kwa upande wa wanaume alikuwa ni Michael Kishimba kutoka JKT Arusha ambaye alitumia muda wa saa 2:29, huku mshindi wa pili Omary Maulidi kutoka Dar es Salaam akitumia saa 2:31, na Jonas John kutoka Singida akishika nafasi ya tatu.

Kwa upande wa wanawake Kilomita 42.2, mshindi wa kwanza alikuwa ni Najim Mwamiko kutoka Dar es Salaam aliyetumia saa 3:32, mshindi wa pili Mtuc Kamili kutoka Dar es Salaam aliyetumia saa 3:51 huku Adventure Lema akishika nafasi ya tatu kwa kutumia saa 3:52.

Kwa upande wa kilomita 21, mshindi wa kwanza kwa wanaume alikuwa ni Mathayo Sombi kutoka Arusha ambaye alitumia saa 1:06, mshindi wa pili Yohana Sule kutoka Arusha ambaye alitumia saa 1:07, wakati Kaposhi Layza kutoka Arusha alishika nafasi ya tatu kwa kutumia saa 1:08. Kilomita 21 kwa upande wa wanawake, Failuna Abdul kutoka Arusha alitumia saa 1:26 hivyo kuibuka mshindi wa kwanza wakati Tunu Andrea kutoka Singida alishika nafasi ya pili baada ya kutumia saa 1:27 huku mshindi wa tatu Neema Sanka kutoka Manyara akitumia saa 1:29.

Mshindi wa kwanza kwa Kilomita 42.2 kwa wanaume na wanawake kila mmoja alizawadiwa Sh. 1,000,000/-, wakati mshindi wa pili akiibuka na Sh. 500,000/- huku mshindi wa tatu akilamba Sh. 250,000/-, na kwa Kilomita 21 mshindi wa kwanza alipata Sh. 500,000/-, wa pili Sh. 250,000/- na wa tatu akazawadiwa Sh. 150,000/ kwa wanaume na wanawake.

Katibu Mkuu wa Goba Road Runners ambao ndio walikuwa wandaaji wa NIC Goba Hills Marathon, Revacatus Kahendaguza, mbali ya kuwashukuru washiriki wote kwa kujitokeza kushiriki mbio hizo, pia aliwashukuru wadhamini wao kwa kujitokeza na kufanikisha mbio hizo huku akifafanua faida zilizopatikana.

# *Fiston wa Yanga atajwa Simba*

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Mtendaji Mkuu wa zamani wa Simba, Crescentius Magori, amesema ilibaki kidogo amsajili Fiston Abdulrazack, ambaye amesajiliwa na Klabu ya Yanga kwenye kipindi cha dirisha dogo na kuwasili nchini wiki iliyopita.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Magori ambaye kwa sasa ni mshauri wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, alisema Fiston si mchezaji mgeni kwao, kwani angekuwa tayari ameshavaa uzi wa Simba siku nyingi kama mambo yangekwenda kama yalivyopangwa.

"Fiston nilitaka kusajili kwenye michuano ya Chalenji liyofanyika nchini Kenya kwenye Jiji la Nairobi na Nakuru. Ile michuano ambayo Zanzibar aliingia fainali mwaka 2017. Alikuja na timu ya Taifa ya Burundi. Tayari tulishakuwa kwenye nafasi nzuri, lakini akapata ofa nono zaidi kwenda nchini Angola, kwa hiyo tulimkosa kidogo tu," alisema Magori.

Magori alisema hayo baada ya madai kuwa klabu ya Simba imekuwa ikichukua wachezaji ambao timu nyingine zimeshaonyesha nia ya kuwasajili, hivyo kuonekana hawana jicho zuri la kuangalia wachezaji mpaka timu zingine zimtaje.

"Si kweli. Hawa wachezaji wote unaowaona wanacheza humu humu Afrika na sisi tunawaona. Sema sisi huwa hatuongei. Tunaongea baada ya usajili," alisema Magori.

Alisema kuwa hata wachezaji Luis Miquissone kuwa baadhi ya klabu wanadai kuwa walitaka kumsajili, lakini wao wakawahi kitu ambacho si kweli, kwani Miquissone wao ndiyo walioanza kumuona kwenye mechi ya kwanza kati ya Simba dhidi ya UD Songo iliyochezwa nchini Msumbuji na kuanza naye mazungumzo.

"Sisi tulianza kuzungumza naye kabla hata hajaja hapa kwenye mechi ya marudiano. Hata Benard Morrison jina lake nililetewa kabla hajaenda Yanga, lakini tatizo rekodi zikaonyesha kuwa hajacheza muda mrefu, tukasubiri kwanza acheze atakakokwenda kucheza kwa miezi sita ili tumuone kwanza. Yeye mwenyewe aliipenda sana Simba baada ya kuiona ikicheza Simba Day dhidi ya Asante Kotoko mwaka 2017," alisema.

# Michezo

Jumatatu Februari 1, 2021

Nipashe





## Solskjaer afurahia sare Arsenal mbio ubingwa

# SIMBA BINGWA SUPER CUP




Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akinyanyua Kombe la Simba Super Cup baada ya kulitwaa jana kwa kutoka suluhu na TP Mazembe ya DR Congo, na kukabidhiwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## ●●● Morrison mfungaji bora, Bwalya mchezaji bora huku Kakolanya akitangazwa kipa bora, safari ya mabingwa yaiva...

**Na Adam Fungamwango**

SAFARI ya Simba kuelekea hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika imeanza vizuri baada ya kutwaa 'Ndoo' ya michuano ya Simba Super Cup iliyomalizika jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Simba imetwaa kombe hilo baada ya sare tasa dhidi ya Mabingwa wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, TP Mazembe, iliyoifanya kufikisha pointi nne ikifuatiwa na Al Hilal ya Sudan ambayo imemaliza nafasi ya pili ikiwa na pointi mbili huku Wongomani hao wakiburuza mkia kwa pointi yao moja.

Mbali na Simba kutwaa kombe hilo ambalo limekwenda sambamba na zawadi ya Sh. milioni 15, wachezaji wake kiungo Rally Bwalya ameibuka mchezaji bora wa mashindano hayo na kukabidhiwa tuzo sambamba hundi ya Sh. milioni mbili huku golikipa Beno Kakolanya akitwaa tuzo ya kipa bora wa mashindano na hundi ya Sh. milioni moja wakati winga Bernard Morrison naye akitunukiwa tuzo ya mfungaji bora iliyoambatana na hundi ya Sh. milioni moja.

Baada ya mechi hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, aliwashukuru Watanzania na mashabiki wote waliojitokeza uwanjani na kuangalia mechi hizo na kusema lengo limetimia.

"Lengo la kuandaa michuano hii ilikuwa ni kuwapa mazoezi na utimamu wa mwili wachezaji wetu, kuangalia wachezaji wapya, lakini pia kuleta burudani kwa mashabiki na Watanzania wote na vyote vimefanikiwa," alisema.

Simba iliandaa michuano hiyo mifupi kwa ajili ya kujiandaa na hatua ya ngazi ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika mechi hiyo ya jana, Simba ilimchezesha mchezaji wake mpya raia wa Nigeria, Junior Lokosa, aliyeingia kipindi cha pili badala ya Rally Bwalya, lakini haikuwa mechi rahisi kama wengi walivyofikiria, kwani kadili muda ulivyozidi kusonga mbele, ndivyo ilivyozidi kuchangamka na kuwa ngumu kwa pande zote mbili.

Ilikuwa ni dakika ya saba tu, wakati kipa wa Simba, Kakolanya alipopiga mpira ambao haukufika kwa mlengwa na kumkuta Isack Tshibangu ambaye alipiga shuti hafifu na kipa huyo kusawazisha makosa yake kwa kuudaka.

Dakika moja baadaye Luis Miquissone akiwa ana kwa ana na kipa wa TP Mazembe, Moukoro Ibrahim, alipaisha mpira juu ya lango.

Dakika ya 19, Simba ilifanya mashambulizi mfululizo kwenye lango la TP Mazembe na kushindwa kuuweka mpira ndani ya wavu, baada ya Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' kupiga shuti lililotemwa na kipa Moukoro, kabla ya kumkuta Miquissone ambaye naye alijaribu kufunga, lakini kipa akipangua na kumkuta Chris Mugalu ambaye shuti lake likadakwa na kipa huyo.

Clatous Chama, yeye alikosa mabao ya wazi, dakika ya 26 alipopiga pembeni na dakika ya 36 alipopaisha pasi safi aliyomegewa na Mugalu.

Kipindi cha pili, pamoja na mabadiliko ya pande zote mbili na kushambuliana kwa zamu, bado hakuna timu iliyoweza kubadilisha ubao wa mabao.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes Da Rosa, alisema hawezi kuwalaumu wachezaji wake kwa kukosa mabao mengi kutokana na ugumu wa mechi, huku Kocha Msaidizi wa TP Mazembe, Isack Kasongo, akisema kuwa walidhamiria kutopoteza tena mechi ya pili.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042



7 708 56 541002 >